Kikao cha Thalathini na Tatu – Tarehe 28 Juni, 2014

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe, Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumini ya Shilingi bilioni mia saba na saba, mia nane na ishirini na tisa milioni, mia sita na arubaini elfu (707,829,640,000) kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia siku ya tarehe 30/06/2015 na kuruhusu utoaji na uhaulishaji wa fedha hizo pamoja na mambo yanayohusiana na hayo. Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Kuanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi na Mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, napenda kuwasilisha mezani Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Wauguzi na Wakunga na Uwazishaji wa Baraza la Usajili wa Wakunga Nam. 9 ya mwaka 1986 na kuanzisha badala yake sheria mpya ya wauguzi na wakunga na mambo yanayohusiana na hayo. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha hati mezani Taarifa ya Utekelezaji wa Haki na Ustawi wa Watoto kwa mwaka 2013/2014. Mheshimiwa naomba kuwasilisha.

Mhe. Mgeni Hassan Juma (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Haki na Ustawi wa Watoto kwa mwaka 2013/2014. Naomba kuwasilisha.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Makisio ya Mwaka 2014

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kwa heshima yako naomba kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015.

Mswada wa Sheria ya Makisio ya Mwaka 2014

(Kusomwa Mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena naomba nitimize wajibu wa kikatiba chini ya kifungu Nam. 106 kinachomtaka waziri mwenye dhamana ya fedha kuwasilisha katika Baraza la Wawakilishi mswada kwa ajili ya kuidhinisha matumizi ya serikali kila mwaka unapoanza. Kwa heshima kubwa naomba sasa na kwa ruhusa yako niwasilishe mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya shilingi bilioni 707,829,640,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha unaoishia siku ya tarehe 30/06/2014/2015 na kuruhusu utoaji na uhaulishaji wa fedha hizo pamoja na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, napenda nianze kwa kukushukuru kwa dhati wewe binafsi na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa mashirikiano makubwa ambayo kwanza yalituwezesha sisi Wizara ya Fedha kuandaa na kuiwasilisha Bajeti ya Serikali ambayo ilipitishwa awali na Baraza lako tukufu.

Pili, katika kuchangia Bajeti za Wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hatimae kumalizia na Bajeti ya Wizara ya Fedha nawashukuru sana kwa mapenzi yenu kwa serikali na wananchi wa Zanzibar bila ya nyinyi kukubali bajeti, sisi watendaji ndani ya serikali tusingeweza kutekeleza majukumu yetu.

Mhe. Spika, napenda pia kulitanabahisha Baraza lako tukufu kuwa mapendekezo ya mswada huu ninaowasilisha umejumuisha makubaliano ya Baraza lako tukufu kuhusiana na marekebisho ya makadirio ya matumizi ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

Mhe. Spika, kuidhinishwa kwa bajeti ya wizara zote hizo kunapelekea Mswada wa Makisio ya Matumizi kutoa uwezo wa kwa serikali kutumia kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina jumla ya shilingi bilioni mia saba na saba, mia nane ishirini na tisa milioni, mia sita na arubaini elfu (707,829,640,000) kati ya fedha hizo shilingi bilioni mia tatu sabiini na sita, mia tano thalathini na nane milioni, mia mbili arubaini na sita elfu (376,538,246,000) kutumika kwa kazi za kawaida na shilingi bilioni mia tatu thalathini na moja, mia mbili tisiini na moja milioni, mia tatu tisiini na nne eflu (331,291,394,000) kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, kupitishwa kwa mswada huu kutaiwezesha pia serikali kukopa ndani na nje fedha kwa ajili ya matumizi ya ndani kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 June, 2015. Kiasi cha fedha kilichoanishwa kwa ajili hiyo ni kama kinavyoongozwa na masharti ya kifungu cha 5 kifungu kidogo (1) cha mswada huu.

Mhe. Spika, mswada huu una vifungu tisa (9).

Kifungu cha 2 kinazungumzia jina fupi. Kifungu cha 2 kinatoa tafsiri ya maneno yaliyotumika katika mswada huu yatakayokuwa na maana sawa na sheria ya fedha za umma Nam. 12 ya mwaka 2015. Kifungu cha 3 kinazungumzia utoaji wa shilingi bilioni mia saba na saba, mia nane ishirini na tisa milioni, mia sita na arubaini elfu (707,829,640,000) kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

Mhe. Spika, kifungu cha 4 kinazungumzia makisio ya fedha zilizokubalika. Kifungu cha 5 chenye vifungu vidogo vinne kinazungumzia uwezo wa kukopa kwa waziri mwenye dhamana ya fedha. Kifungu cha 6 chenye vifungu vidogo vitatu kinazungumzia uwezo wa waziri katika maombi ya ziada kwa lengo la kukabili matumizi mengine ya dharura pale haja itakapojitokeza.

Mhe. Spika, Kifungu cha 7 kinazungumzia marejesho ya mkopo na riba. Kifungu cha 8 kinazungumzia kukubaliwa kwa mpango wa maendeleo na Kifungu cha 9 ambacho ni cha mwisho kinazungumzia kukubaliwa kwa fedha zitakazopitishwa kwa matumizi ya maendeleo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi ya mswada huo naomba sasa kwa idhini yako kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe kuujadili na hatimae kuupitisha mswada huu ili uwe sheria ya matumizi ya serikali kwa mwaka wa fedha 2014/2015. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe hoja imeungwa mkono, kimsingi kazi hiyo Waheshimiwa Wajumbe mumeshaifanya. Mmeifanya kazi hii kuanzia tarehe 14/05/2014 na mjadala ukaendelea hadi jana mkamaliza shughuli hiyo, lakini hata hivyo kwa kuwa huu ni mswada basi naomba nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti, wa Kamati ya Wenyeviti Mhe. Hamza Hassan Juma kama ana jambo lolote kuhusiana na mswada huu.

Mhe. Hamza Hassan Juma (Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti): Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii nikiwa kama Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti kuja kusoma Mswada wa Kuidhinisha Makisio ya Matumizi ya Shilingi bilioni (707,829,640,000) kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia siku ya tarehe 30 June, 2014/2015. Na vile vile kuruhusu utoaji na uhaulishaji wa fedha pamoja na mambo mengine.

Mhe. Spika, kwa kutumia uzoefu wa siku nyingi wa kuwepo katika Baraza hili la Wawakilishi kwa kweli mimi na wenyeviti wenzangu hatuna matatizo kwa sababu bajeti kuu ya serikali tuliipitisha kwa kauli moja pamoja na ushauri ambao tuliutoa kwenye kamati kwa kumshauri Mhe. Waziri, kwamba katika bajeti inayokuja basi angalau tuwe na utaratibu wa ile bajeti ya serikali katika hali ya maandalizi tuweze kukaa pamoja, ili kuhakikisha kwamba kile tunachokuja kukipanga kwenye bajeti tusije tukaanza kulalamika kwenye mafungu ya wizara mbali mbali.

Mhe. Spika, pamoja na kuyakubali matumizi haya ya kutoa fedha katika Mfuko Mkuu wa Serikali lakini tu nilikuwa nataka nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa sababu nimeangalia hiki kifungu cha 6(1) cha huu mswada naomba Mhe. Spika kwa ruhusa yako niweze kukinukuu kinasema;

> "Waziri mwenye dhamana na mambo ya fedha ikiwa ataona ni muafaka kwa Taifa kutoa matumizi ya ziada kwa Wizara au Idara yoyote ya Serikali ikiwa ni zaidi ya fedha zilizokubalika kwa matumizi yaliyokusudiwa au kwa madhumuni ya huduma nyengine yoyote na itakuwa ni hasara kwa Taifa kusubiri mpaka pale zitakapotolewa tena na Baraza la Wawakilishi, bila ya kujali masharti ya sheria hii au sheria nyengine yoyote anaweza kuidhinisha matumizi ya ziada ambayo yatatumika kwa mujibu wa kasma inayohitajika"

Kifungu 6(2) kinasema;

> "Waziri mwenye dhamana na mambo ya fedha atakapoidhinisha maombi ya kiasi chochote cha fedha chini ya kifungu hiki mara tu baada ya kuruhusu maombi hayo ya ziada atawasilisha nyongeza ya makisio hayo mbele ya Baraza la Wawakilishi kwa maelezo ya nyongeza hiyo kama hali itakavyokuwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu 106 (2) ya Katiba ya Zanzibar, 1984 ikiwa ni nyongeza ya matumizi ya ziada."

Kifungu 6(3) kinasema;

> "Waziri mwenye dhamana ya mambo ya fedha anaweza kukasimu uwezo wake alionao chini ya kifungu hiki kwa afisa yeyote kwa mujibu wa masharti atakayoona yanafaa."

Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba kuna utaratibu za matumizi ya fedha kutoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali na mimi mwenyewe nilipokuwa nikichangia katika hotuba ya Wizara ya Habari nilieleza *concern* yangu na nilitaka maelezo ya kina kuhusu fedha zile karibu bilioni 6 ambazo zilitoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali, lakini taarifa yake Mhe. Waziri wa Fedha hakuwahi kutuletea Barazani kwa ajili ya kutoa taarifa kwa Baraza, lakini vile vile kuridhia matumizi yale. Kama sheria inavyosema kwamba kama itaonekana bila wa waziri kutoa fedha zile au kuruhusu fedha zile kutokana katika Mfuko Mkuu wa Serikali waziri anaweza akatoa fedha zile na baadae kutoa taarifa kwa Baraza.

Sasa jambo hili kwa kweli halikufanyika na ndio maana nikajaribu kushauri kwamba iko haja yakupata taaluma kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kupitia Afisi ya Mwanasheria Mkuu au mwenyewe Mhe. Waziri wa Fedha, ili wajumbe waweze kuelimishwa kile kifungu cha Katiba hasa kilikusudia nini. Hii sheria ya kutoa fedha katika Mfuko Mkuu wa Serikali madhumuni yake hasa imekuwa nini, kwa sababu tumekuwa tukishuhudia kwamba fedha zinatoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali lakini kwa zile sheria maalum ambazo tumezitunga. Kwa mfano, kama mafao ya viongozi wakuu wa Kitaifa.

Kwa hiyo, yale Mhe. Waziri anaweza kutumia fedha katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa sababu tayari katika ile sheria ya viongozi wa kitaifa tulikwisha kuruhusu kwamba mafao yale yaweze kutumika kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina. Lakini kwa bajeti nyengine za serikali ukiacha ile bajeti ambayo tuliyoidhinisha hapa Barazani, basi fedha yoyote ya ziada itakayotolewa, ili kufanya matumizi ya ziada, basi lazima taarifa ile ilikuwa ije kwenye chombo hiki ili kuweza kupata Baraka. Kwa kuwa matumizi yanakuwa ni mazuri hatutegemei kwamba Baraza la Wawakilishi linaweza likaja likamkatalia Waziri wa Fedha kwa ajili ya kutumia fedha za ziada katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, nadhani kama nilivyosema kwamba bajeti hii tumeshaipitisha na sitegemei kama kuna mjumbe yeyote atakayekataa mswada huu, kwa sababu kama hatujaidhinisha matumizi ya fedha basi hata hiyo bajeti yote tuliyoipitisha hapa kazi yetu itakuwa bure. Kama tunavyofahamu tuna miradi yetu mbali mbali katika majimbo,

kuna miradi ya kitaifa, kuna huduma vile vile za jamii zinatakiwa zitolewe na serikali na sasa hivi wenzetu katika wizara zote tayari wameshafunga mahesabu yao, wameshafanya marejesho yao na wanasubiri sasa ikifika tarehe 1 Julai ndio waanze kufanya tena matumizi. Kwa hiyo, ikiwa sisi Mswada huu tutaukataa leo basi serikali itabidi iende likizo mpaka kiitishwe kikao cha dharura kwa ajili ya kuja kuruhusu sasa matumizi ya fedha ya serikali.

Kwa hiyo, baada ya hayo machache naamini na wenzangu wengine watapata nafasi ya kutia nyama katika mswada huu. Lakini pia naamini mswada wenyewe ni mfupi tutaweza kumaliza kwa haraka sana.

Mhe. Spika, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura tunaunga mkono mswada huu wa serikali, ili wananchi wakaweze kupatiwa huduma zile ambazo zilikuwa zikitarajiwa. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Wenyeviti. Bado naendelea kuwaomba Wajumbe wanaotoka kwa dharura warudi tumalize kazi hii. Hii ni kazi inayohitaji uamuzi, kufeli kwetu hapa maana yake serikali haiwezi kutumia. Naomba sana Wajumbe walioko nje waingie ndani ili tuifanye kazi hii. Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa.

Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa: Ahsante Mhe. Spika, kwa asubuhi hii ya leo na mimi kunipa fursa nikawa mtu wa kwanza kuchangia katika Mswada huu muhimu ambao umewasilishwa katika Baraza hili tukufu.

Vile vile nachukua fursa hii kumshukuru Waziri wa Fedha pamoja na timu yake yote ya watendaji ikiongozwa na Katibu Mkuu kaka yangu, Khamis Mussa Omar kwa kazi kubwa na nzito ambayo wameifanya hadi leo hii tukafikia tamati katika suala zima la kupitisha *Appropriation Bill*.

Mhe. Spika, mimi kwangu kwa siku ya leo nyingi ni shukurani. Natoa shukurani zangu za dhati kabisa hususan baada ya kumsikia Mhe. Waziri alipokuwa akisoma hotuba yake hapa kwa siku ya leo kutilia maanani na kuchukulia hatua suala zima la yale marekebisho ya fedha ambayo ilikuwa tumeyafanya katika Baraza hili tukufu.

Mhe. Spika, napenda vile vile kuchukua fursa hii kuwapongeza sana wizara hii kwa kazi nzito ambayo wameifanya, pia kama ambavyo tumesikia katika vyombo vyetu vya habari leo asubuhi kuwa kuna watu walijaribu kutaka kufanya ubadhirifu na wizi katika Mfuko Mkuu wa Hazina. Lakini kwa umakini wao wakaweza kudhibiti hali ile na kabla ya tukio lile ambalo lingeathiri nchi yetu kwa wizi wa *Euro* milioni mbili , zikaweza kudhibitiwa na hatimaye suala hilo likawa katika mikono ya sheria.

Mhe. Spika, la zaidi katika hayo ningelipenda kumuelekeza Mhe. Waziri kwamba, katika mwaka huu wa fedha ambao tunamalizia leo kuna matatizo ambayo yalijitokeza hususan katika vile vitabu vyetu vya bajeti. Namuomba Mhe. Waziri suala hili atakapokuja tena kwa mwaka wa fedha unaofuata tuhakikishe kwamba linafanyiwa utaratibu na yale mafungu ambayo yalikuwa yanaleta utata yawe yanaangaliwa vizuri, na wawe na utaratibu wa kufanya uhakiki wa mwisho kabla ya vitabu vile kuletwa katika Baraza lako hili tukufu.

Vile vile Mhe. Spika, ningelimuomba Mhe. Waziri ule utaratibu ambao tulikuwa tumeutumia mwaka huu wa kuleta vitabu kwa wizara, nahisi ingekuwa ni jambo la msingi na jambo la busara tukarejea utaratibu wetu ule ule wa zamani kitabu kikawa kimoja tu, badala ya kutengeneza vitabu vidogo vidogo baadae tukaja tukatengeneza kitabu kimoja kikubwa ambacho kwa mfumo wetu wa mara hii kilionekana kina matatizo ya hapa na pale.

Baada ya maelekezo hayo Mhe. Spika, mimi naunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja hususan baada ya marekebisho ya kina ambayo yalikuwa-*raised* hapa na Mwakilishi mwenzetu Mhe. Ismail Jussa Ladhu na baadae Mhe. Waziri akayafanyia kazi vizuri na nimeyaona katika maelekezo yetu humu. Baada ya hayo Mhe Spika, nashukuru sana na ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuwepo asubuhi hii ya leo katika kutekeleza majukumu yetu. Pia naendelea kutoa shukurani zangu kwa kutujaalia kipindi chote hiki; tokea mwanzo wa bajeti hii mpaka leo tunafikia ukingoni tukiwa tunaelekea Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, Mwenyezi Mungu atujaalie afya njema na umri mzuri wa kuweza kuifunga Ramadhani hii na iwe yenye kukubaliwa.

Baada ya hapo nikupe wewe nafasi ya kukupongeza vile vile kunichagua kuwa miongoni mwa wasemaji katika mswada huu. Pia nimpongeze waziri kwa kuwasilisha mswada wake huu vizuri.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu katika mswada huu kwa kweli ni mchango mfupi sana, lakini ufupi wake ni kuutaja tu, maana yake ni kubwa sana. Kwa kweli mimi ninasikitika sana na watumizi wa hizi fedha. Katika kitu ambacho nataka kukizungumzia ni kwamba tumepitisha Miswada mbali mbali na kuidhinisha vifungu mbali mbali vya matumizi, sasa sisitizo langu kwa watendaji wanaohusika na matumizi ya fedha wazitumie fedha kwa mujibu wa vifungu vinavyotakiwa na kwa mujibu wa taratibu na sheria za fedha za Zanzibar.

Mhe. Spika, inasikitisha sana kuona kwamba fedha baada ya kuziidhinisha katika Baraza la Wawakilishi na kuingia katika Mfuko Mkuu wa Hazina na kuingizwa katika wizara mbali mbali zinakutiwa kasoro mbali mbali za matumizi ya fedha hizo. Namuomba Mhe. Waziri awe makini sana katika watendaji ambao wamepewa dhamana ya fedha wazitumie fedha hizi kwa uaminifu na uadilifu na kwa malengo yale yaliyokusudiwa.

Inasikitisha Mheshimiwa kuona kwamba zinapita kamati katika shughuli za kukagua fedha na matumizi unakuta fedha zimetumiwa hazina vielelezo. Fedha zimetumiwa kinyume na taratibu, hili ni tatizo kubwa. Namuomba Mhe. Waziri awe makini sana kwa watendaji hawa ambao wanakwenda kinyume na taratibu za sheria na matumizi ya fedha za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa mchango wangu huu mdogo na mimi niseme kwamba naiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja, nikiwatakia mafanikio mema na utendaji mzuri na wa uadilifu watendaji wote wanaohusiana na Wizara ya Fedha. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Spika, nami kupata nafasi ya kutoa mawili tu, kama yatafika. Kwanza nikushukuru wewe nami kunipa nafasi, nimpongeze Mhe. Waziri na wetendaji wake kwa kutuletea mswada huu ambao ni hitimiso la kazi kubwa tuliyoifanya katika kuchangia Bajeti ya Serikali na wizara tofauti. Leo hapa kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu tunahitimisha na tunaingia katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, bajeti hii itaanza matumizi yake katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Kwa hivyo, kwa kuwa tunaingia katika Mwezi Mtukufu ningeomba kuwe na ubunifu wa kutumia fedha hizi.

Mhe. Spika, bajeti hii inaonesha matumizi ya kawaida ya serikali na yale matumizi ya maendeleo. Kwa kawaida matumizi ya maendeleo mara nyingi ndio fedha yake inayochotwa, hapa fedha hiyo ya maendeleo sio nyingi kiasi hicho. Niungane na msemaji aliyepita Mhe. Mohammed Mbwana Hamad kuwataka wenzetu, watendaji wetu wawe waadilifu wanapotumia fedha hizi hususan hizi za maendeleo, ili ile miradi ya maendeleo na programu zilizopangwa ziweze kutekelezeka kulingana na fedha itakayopatikana.

Mhe. Spika, fedha hii ya maendeleo ni ndogo na nchi yetu inahitaji kupata maendeleo, kwa kawaida nchi kila inapokua, ipate maendeleo makubwa. Kwa hivyo, hizi fedha chache ambazo tumeziidhinisha na leo tunamaliza kuziidhinisha zitumike kwa niaba ya miradi iliyopangwa na kusitokezee udokozi wa aina yoyote, ili Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mara hii kwenye bajeti hii iwe hakuna dosari ya matumizi ya fedha hizi.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, kwa kuwa bajeti yote tumeunga mkono hakuna haja yoyote nyengine ya kusema mtu kuwa siungi mkono, kwa sababu itakuwa hatujui tufanyalo. Baada ya hayo naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja na Waziri wa Fedha na watendaji wake nawatakia wawe waadilifu katika kutumia fedha hii ambayo tunaidhinisha leo hapa. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, mimi kwanza naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa leo hii kutufikisha salama na pumzi za dakika hizi za 90 bado tunaendelea kupumua, hilo moja. La pili, nikushukuru na wewe na nikupe pole na safari yako uliyorudi.

Mhe. Spika, nilimsikia Mhe. Hamza Hassan Juma, Mwenyekiti wa Wenyeviti na alituasa sana kuwa ataona ajabu kuwa Mjumbe kutokezea kuupinga mswada huu na kwa kuwa huko nyuma tumeshaanza kukubali bajeti yote.

Mhe. Spika, mimi nakubaliana nalo hilo, lakini na yeye Mwenyekiti wa Wenyeviti atupe ruhusa angalau kama kuna vifungu tumeona vinatakiwa tuvisaidie ili sheria iweze kufanya kazi yake vizuri. Naomba hilo.

Mimi sina hoja kubwa mbele ya mswada huu lakini binadamu kutoa tahadhari ni lazima, na binadamu wenyewe ndio sisi hatukawii kugeuka, leo tukawa hivi, kesho tukawa vile. Nimejaribu kuangalia sana sijaona sheria ambayo inatakiwa Mhe. Waziri apewe fursa ya kufanya hivyo, pia sijaona sheria ambayo itakayomlinda yeye kwenye mswada huu. Naomba sana Mhe. Waziri atapokuja anioneshe jinsi gani waziri kuna mambo anaweza akafanya kwa kuwa tumeshampa *power* ya kuweza kufanya mkopo, kuweza kutoa fedha ambazo kiasi kilichokubalika humu. Nina wasi wasi, leo waziri huyu mzuri lakini mwengine hatoweza kutumia vizuri *power* hii na hasa kuwa kuna fedha za maendeleo ya jamii, akatumia vile anavyotaka yeye mwenyewe kwa kuwa tumempa *power*.

Mhe. Spika, mswada huu nimeufurahia sana umekuja wakati muwafaka, kwa sababu hivi sasa mawizara yote yameshafunga mahesabu yao. Lakini kuna wengine ambao wananchi huwa wanapata matatizo ya kuweza kulipwa mafao yao ndani ya ile wizara husika. Sasa mimi nimefurahi sana kuwa kwa kuwa Mhe. Waziri tunampa *power* hii, basi namuomba sana katika Wizara ya Afya kuna mtu ambaye anadai pesa zake na wakati muda huu sio pahala pake kwa kuwa fedha zote zishawekwa, basi naomba kwa kutumia *power* hii waweze kumuidhinishia yule katibu, ili aweze kulipwa pesa zake yule mtu.

Mhe. Spika, kwa hayo machache mimi niunge mkono mswada huu kwa asilimia mia moja, ahsante sana.

Mhe. Ali Mzee Ali: Mhe. Spika, na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia kuwa mzima leo. Vile vile nikushukuru na wewe kunipa nafasi hii. Leo tunaweka historia ndani ya Baraza hili. Mwaka 1980 Baraza la Wawakilishi lilianzishwa rasmi, napenda niwatambue wale ambao siku ile Baraza hili linaanzishwa ambao leo bado wamo humu ndani na hakuna mwengine isipokuwa Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban, ambaye hivi karibuni kapewa cheo cha usharifu. Huyu ni mzoefu na ni fahari yake kuwa leo yupo hai hapa anashuhudia mambo haya.

Leo kwa nini tunaweka historia? Kwa sababu leo tunatekeleza katiba iliyompa madaraka waziri anayeshughulikia fedha kuleta hoja humu ndani inayosema; kuidhinisha makisio na matumizi ya serikali ambayo tumeyajadili. Ni mara ya mwanzo katika miaka 35 kabla ya tarehe 1 Julai, tunapitisha na tarehe 1 Julai, tunatekeleza jambo ambalo katiba kwa miaka yote ilitaka tufanye na mwaka huu tunafanya.

Mhe. Spika, napenda kuipa pongezi serikali nampa pongezi na Mhe. Waziri, miaka yote uliokuwa humu ndani Julai 5, 6, 7, ndio *some time* mpaka kati kati, lakini safari hii kwa mara ya mwanzo tarehe mosi matumizi yanatumika kisheria. Sifa hiyo naomba iende kwa Dkt. Ali Mohammed Shein. Miaka 10 iliyopita Wizara ya Fedha ikiongozwa na Rais na mawaziri wa Nchi Ofisi ya Rais, aliongoza Mhe. Suleiman Othman Nyanga, Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini. Awamu hii ya Saba kwa miaka mitatu wizara hii iliongozwa na Waziri wa Nchi (OR) Fedha na Agosti mwaka jana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi amempima, amemuangalia, ameona sasa inabidi aondoshe dhamana ile kwake na amkabidhi Mhe. Omar Yussuf Mzee, aiongoze wizara hii kuwa Waziri wa Fedha kamili. Mheshimiwa nakupongeza sana. *(Makofi)*

Rais hajakosea, jana umeona namna bajeti yake ilivyopita hakuna buti isipokuwa shukurani na mimi Mheshimiwa nakupa shukurani. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Fedha huyu ni mzoefu, amekuwa mtu wa takrimu, amekuwa Katibu Mkuu wa Mipango na waziri wake Mhe. Ali Juma Shamhuna kamlea, kawa nae, awamu ya sita akawa Katibu Mkuu Waziri Kiongozi, baadae akawa Mbunge akaenda Bara, akawa Naibu Waziri wa Ulinzi, Naibu Waziri wa Fedha, na mwaka 2005 Rais akamteua akapata dhamana hii. Naomba tumeidhinishie bajeti hii, bajeti aina yake haijapata kutokea, lakini bajeti hii inataka kufuatiliwa na naamini tukimsaidia na yeye mwenyewe lazima bajeti inayokuja aoneshe mabadiliko na uwezo wa mapato.

Fedha ya Serikali inatumiwa vibaya, matumizi mabaya, watu wanafanya wanavyotaka. Sasa sisi kama Wawakilishi na kama ndio ngome ya wananchi tunaahidi, na mimi nasema kwa niaba ya wote tutasimamia kuziba mianya yote. Wewe Mhe. Spika, ukiongoza Baraza hili ningekuomba sana, tuanze sisi wenyewe chombo chetu hiki kubana matumizi kuanzia tarehe 1 kesho kutwa. Naamini kwa uadilifu wako, kwa kupenda haki utasimamia hilo bila ya wasiwasi wowote.

Mhe. Spika, naiomba Serikali kwa sababu kesho tutaanza mwezi mtukufu wa Ramadhan, Mwenyezi Mungu atujaalie kwanza tuifunge Ramadhan hii kwa salama na amani na zote siku 30 tuzifunge. Kesho tutakuwa na

mafunzo ya mambo ya zakka, tutoe zakka. Naiomba Serikali isimamie bei za vitu, na nawaomba waislam wafanyabiashara wawe na huruma katika mwezi huu wa kheri.

Mhe. Spika, la mwisho mimi naunga mkono mswada huu asilimia mia kwa mia. Mhe. Spika, naomba zaidi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi Mwenyezi Mungu atujaalie tuondoke salama, tukafunge salama, tukutane tena Agosti kwenye Bunge la Katiba. Tukirudi Oktoba Mwenyezi Mungu ajaalie tuunde Katiba Mpya ya Tanzania yenye manufaa na Zanzibar. Mwenyezi Mungu atujaalie kila la kheri.

Mhe. Spika, kwa hayo mafupi napenda kumalizia kuwashukuru Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kipindi chote hiki walichochangia kwa makini, kwa umoja, na Mwenyezi Mungu atujaalie umoja wetu huu tushikamane nao twende mbele. Mhe. Spika, naomba kumalizia.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu. Mhe. Spika, pili nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi. Mhe. Spika, mimi kama nilivyosema kwamba nitatumia muda mdogo sana wa kuchangia katika mswada huu.

Mhe. Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote. Kama alivyosema Mhe. Ali Mzee Ali kwamba ni kwa mara ya kwanza, na kweli ni kwa mara ya kwanza. Ina maana kwamba Serikali yetu inapiga hatua kubwa sana na hili kwa kweli tulipongeze.

Mhe. Spika, mimi kidogo ningegusia tu suala ambalo amelizungumza Mhe. Ali Mzee Ali, kuhusiana na matumizi yetu ya fedha ambayo yanatumika vibaya sana. Ningeomba sana Mhe. Waziri kulisimamia hili kwa sababu kuna matatizo makubwa; kwanza katika uvujaji wa mapato yetu katika maeneo mbali mbali, pia na matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Kwa hivyo, Mhe. Waziri ningekuomba kwa hilo ulisimamie.

Mhe. Spika, mimi kidogo nilikuwa nataka kumuomba Mhe. Waziri wa Fedha, kwa sababu moja katika fedha ambazo zinaingia ni fedha za wafadhili, na fedha hizo zinaingia katika maeneo mbali mbali. Sasa Mhe. Spika, katika Wizara ya Fedha kuna kitengo kinaitwa *Aid Coordination* ambao wao wanakusanya fedha za wafadhili zinazoingia katika AZAKI za Kiraia. Ningemuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha kwa sababu hili pia ni jukumu lao kuangalia vizuri fedha zile zinazoingia. Bado kunaonekana kwamba kuna baadhi ya fedha zinaingia katika AZAKI za Kiraia lakini hazijulikani zinakwenda wapi, zinatumiwa vipi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri naomba hili muendelee kulisimamia, najua kipo kitengo hicho kinafanya kazi, lakini bado kuna AZAKI ambazo hazipeleki ripoti. Mhe. Waziri nakuomba sana hilo ulisimamie.

Jengine Mhe. Spika, miradi yetu mingi pia tunapata fedha kutoka kwa mashirika ya kimaendeleo. Mhe. Waziri nilikuwa nakuomba sana tusimamie fedha ambazo zinakuja kwa jina la Tanzania kwamba na sisi kama Zanzibar tupate sehemu ya fedha hizo, kwa sababu bado kumekuwa kuna utata ndani ya kupata fedha hizo ambazo na sisi zinatusaidia katika maendeleo yetu.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Waziri kuna fedha ambazo zinaitwa *Obama Power Initiative.* Ningeomba Mhe. Waziri uje utuletee taarifa fedha hizo ambazo zitaingia kwa jina la Tanzania kwa upande wa Zanzibar tutapata kiasi gani, au tutapata asilimia ngapi ili na sisi ziweze kutusaidia katika miradi yetu ya maendeleo, hususan miradi ya umeme.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa fursa hii na mimi pia naunga mkono mswada huu kwa asilimia mia moja na nawaomba wenzangu waunge mkono. Mhe. Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii adhimu ya kuchangia mswada huu. Nichukue fursa ya pekee na mimi kumshukuru mume wangu kwa kipindi chote hiki cha bajeti hii, kwa kunivumilia kwa kuweza kufika hapa kwenye Baraza hili tukufu na kufanya kazi ile ambayo tumetakiwa kuifanya.

Mhe. Spika, kwa kweli hili ni jukumu letu kwa mujibu wa sheria. Sisi ni Wawakilishi wa wananchi na ni jukumu letu kutimiza ahadi hii. Kwa sababu tumefanya kazi nzito kwa muda mrefu na hapa tumefikia mwisho wa kazi hii, ni lazima tuupitishe mswada huu kwa asilimia mia kwa mia. Nashukuru kwa hilo.

Mhe. Spika, kwa kuwa fedha hizi ni za Serikali, kwa hivyo ile mikataba basi naomba iwe mikataba mizuri na yenye kutekelezeka. Zile fedha za miradi vile vile, miradi ambayo itakuwa endelevu na kuiletea faida kwa wananchi wetu.

Mhe. Spika, nikienda kwenye kifungu cha 5 Uwezo wa Waziri kukopa. Waziri mwenye dhamana ya mambo ya fedha anaweza kukopa wakati wowote ule lakini sio zaidi ya tarehe 30 Juni, 2015 ikiwa ndani au nje ya Zanzibar kiasi chochote cha fedha ambacho hakitozidi kiasi kilichokubalika.

Mhe. Spika, hapa nimuombe Waziri kwamba hizi fedha za mikopo kwa sababu kukopa kuna mashaka yake, kuna kupata na kukosa. Hizi fedha ambazo anazikopa basi ziwe na masharti nafuu.

Vile vile nikienda na kifungu cha 7; kiasi cha fedha kitakachohitajika wakati wowote kama malipo ya riba kuhusiana na fedha mwaka 2014/2015 shilingi 22,512,482,000/=, hiki ni kiwango ambacho amekiweka hapa. Nimuulize tu Mhe. Waziri ana uhakika gani wa kuzipata fedha hizi za mikopo na ambazo ameshaziweka pamoja na riba yake. Mhe. Spika, naomba Mhe. Waziri akija anifahamishe hilo.

Mhe. Spika, naunga mkono asilimia mia kwa mia mswada huu.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuchangia Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Bilioni 707,829,640,000/= kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia siku ya tarehe 30 Juni.

Mhe. Spika, mimi nitakuwa na maombi na ushauri tu katika mswada huu. Mhe. Spika, kwanza nimuombe Mhe. Waziri kuwepo na usimamizi mzuri wa mapato haya.

Pili kuwepo na kudhibiti uvujaji wa mapato, tatu kuangalia zaidi vianzio vyengine vya mapato, ili kuweza kusaidia shughuli za maendeleo mbali mbali katika nchi yetu.

Mhe. Spika, katika suala la fedha za wafadhili nilikuwa namuomba Mhe. Waziri. Hizi fedha za wafadhili ni mikopo ambayo tunasaidiwa kutoka na nchi mbali mbali. Kwa hivyo, nilikuwa naiomba tu Serikali kupitia Wizara hii, hizi fedha zinahitaji kulipwa na walipaji ndio walipa kodi wetu. Sasa nilikuwa naomba tu zisimamiwe vizuri, zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa ili kuleta tija katika nchi yetu.

Mhe. Spika, la mwisho nimuombe Waziri wa Fedha hizi ziweze kuingizwa kwa wakati katika Mawizara tofauti, ili shughuli zile ambazo zimepangwa zitumike kwa wakati uliokusudiwa. Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kwa heshima kubwa kwanza nataka nianze kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa michango yao. Nina imani kubwa kwamba michango waliyoitoa ni kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi zaidi. Mimi ninaelewa kwamba wengi walitaka kuchangia lakini kutokana na muda hawa waliopata kuchangia basi walikuwa na uwakilishi wetu sote. Naomba basi kama kawaida yetu niwataje wale ambao wamechangia.

Mhe. Spika, waliochangia leo katika mswada huu ni Wajumbe tisa, na wote wamechangia kwa kusema, hakuna aliyechangia kwa maandishi.

1. Mhe. Hamza Hassan Juma
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
3. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
4. Mhe. Mohammed Haji Khalid
5. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
6. Mhe. Ali Mzee Ali
7. Mhe. Mgeni Hassan Juma
8. Mhe. Fatma Mbarouk Said
9. Mhe. Marina Joel Thomas

Mhe. Spika, mimi binafsi na kwa niaba ya watendaji wakuu wa Wizara ya Fedha tunawashukuruni nyote kwa ujumla.

Mhe. Spika, kwa sababu Wajumbe waliochangia ni wachache, naomba basi nitoe ufafanuzi juu ya michango yao.

Kwanza nataka kwa ujumla niseme mambo mawili ambayo yamechangiwa karibu na Wajumbe wote.

La kwanza, ni shukrani na pongezi ambazo mlizotupa. Kwa niaba ya watendaji wa Wizara ya Fedha tumezipokea na nataka nikwambieni. Shukrani ambazo mumetupa sisi na sisi tunazirudisha kwenu, ili zipelekwe kwa wananchi wote wa Zanzibar. Tunaelewa fika kwamba utekelezaji mzuri wa bajeti yetu hii umetokana na wananchi wetu wa Zanzibar kuwa watulivu, wenye uadilifu, na wenye imani kubwa na Serikali yao. Kwa hivyo, na sisi tunawapongeza sana wananchi wa Zanzibar.

La pili, ni lile suala ambalo limeulizwa, au limetolewa ufafanuzi; limesisitizwa na Waheshimiwa Wajumbe karibu wote, suala la kusimamia vyema fedha za Serikali. Nataka nikuahidini kwamba tumelipokea kwa mikono miwili na tutasimamia kwa nguvu zetu zote. Pale ambapo Waheshimiwa mtakapoona kwamba hapa hatwendi vizuri, sio ndani ya Wizara ya Fedha tu, ndani ya Serikali kwa ujumla wake, nakuombeni sana mtuarifu, ili tuweze kuchukua hatua mapema zaidi. Mkichelewa kutuarifu tutakuja kupata maharibiko na yale maharibiko yatakuwa ni yetu sote, hayatakuwa kwa Serikali tu peke yake, yatakuwa hata kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi wetu kwa ujumla. Nakuombeni sana mtuarifu mapema ili tuweze kuchukua hatua.

La tatu, ni lile suala ambalo nalo limezungumzwa na karibu Wajumbe wote, suala la kudhibiti uvujaji wa mapato. Tutajitahidi sana, kila ambapo tutakapoona pana harufu ya uvujaji tutajitahidi basi kupeleka nguvu zetu zote tuweze kudhibiti. Kama walivyosema baadhi ya Wajumbe wakati wa mijadala kwamba kazi hii ni kazi vile vile ya Baraza la Wawakilishi, tusaidiane katika suala hili, tusaidiane muwe mnatoa taarifa.

Mhe. Spika, nashukuru katika michango tumeweza kutoa taarifa nyingi sana kupitia Wizara mbali mbali. Tumezichukua, watendaji wa Wizara ya Fedha walikuwepo toka bajeti imeanza mpaka siku ya mwisho ili kuchukua yale ambayo yanatufanya sisi tuweze kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi zaidi.

Nashukuru kuna maeneo mengine mmemkabidhi Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi ili aweze kuyafanyia kazi. Nina imani kubwa kuwa Mtendaji wetu Mkuu kwa uadilifu wake na kwa utendaji wake na yeye atayafanyia kazi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya ujumla, sasa naomba basi niende kifungu kimoja baada ya kimoja. Kwanza Mhe. Hamza Hassan Juma nataka niseme kama yafuatayo. Waziri mwenye dhamana ya fedha ametakiwa kufanya mambo mawili. Nataka nikuhakikishie Mhe. Spika na Baraza lako tukufu kwamba tutaanza kuyatekeleza kila itakapokuwa ni lazima tuyafanye. Kwa mujibu wa Sheria ya Fedha, Idara yoyote au Wizara yoyote itakayozidisha makisio yaliyopitishwa na Baraza lako tukufu katika matumizi, ikionekana kwamba ni lazima, Waziri mwenye dhamana ya fedha anatakiwa kutoa taarifa ndani ya Baraza lako tukufu. Tutafanya hivyo kwa mujibu wa Sheria ya Fedha.

Pia kwa mujibu wa katiba kifungu cha 106 Waziri mwenye dhamana ya fedha, ikiwa Serikali nzima itataka kutumia fedha za ziada ya ile bajeti ambayo iliyopitishwa, tunatakiwa tuje tuombe idhini ya Baraza la Wawakilishi. Hapa tunatakiwa tuombe idhini. Katika miaka yangu minne ya Uwaziri wa Fedha bado sijazidisha, nitakapozidisha nitakuja kuomba idhini.

Ombi la Mhe. Hamza Hassan Juma la kutaka angalau tuelimishane katika kifungu kile cha katiba, basi na mimi nitamuandikia Mhe. Mwanasheria Mkuu barua rasmi ya kuomba ombi hilo. Na yeye basi atatafuta wakati muafaka ili tuje tuelimishane kifungu kile cha katiba na vifungu vyengine vilivyomo ndani ya katiba yetu, ambavyo vinamuongoza Waziri wa Fedha afanye nini kikatiba. Nitamuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu ili atusaidie kwa hilo. Kwa sababu kila mmoja ana wadhifa wake na nafasi yake katika kuieleza jamii yetu, nini tunatakiwa kutekeleza ndani ya Serikali yetu.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa shukrani tumezipokea na amesema marekebisho ya fedha ambayo tuliyoyafanya. Mhe. Spika, utakumbuka kwamba tulipozungumzia Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kuna shilingi karibu milioni 50 hazikuwa na maelezo. Tumetakiwa tuzihamishe tuzirudishe Mfuko Mkuu wa Serikali.

Pia tulipozungumza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kulikuwa kuna karibu milioni 500 na kitu katika vifungu vile vilivyowekwa vya maposho ambavyo havistahiki maposho ya ualimu. Kama mnakumbuka tumetakiwa navyo vile vile tuvipeleke kwenye mikopo ya elimu ya juu. Nimeyataja katika hotuba yangu maeneo hayo mawili tumeyachukua na tutayafanyia kazi ili kuona kwamba fedha zile zinakwenda kule ambako Baraza lako Tukufu Mhe. Spika, ulipoelekeza.

Hii ni kwa mujibu wa uwezo wa Baraza la Wawakilishi waliopewa ki-Katiba. Kwa hivyo, na sisi tunakwenda na tayari Baraza limeshatuarifu na tayari tumeshaanza kuzifanyia kazi. Ninamshukuru Katibu wa Baraza ametuletea barua siku ya pili tu kutuarifu hayo maelekezo ya Baraza la Wawakilishi. (*Makofi*)

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa vile vile umetaka marekebisho ya vifungu. Ninadhani suala hili vile vile limekuwa-*echo* na Mhe. Mgeni Hassan Juma. Tayari tumeshampa maelekezo Kamishna wa Bajeti, baada ya kumaliza tu akae na timu yake wapitie vifungu vyetu vyote. Kuna vifungu vipo pale, pesa zake hazina tafsiri na kile kifungu. Tunataka vifungu hivyo avifanyie kazi, aviweke vizuri zaidi.(*Makofi*)

Kuna vifungu havina maana tena kukaa katika buku letu, aviangalie ni jinsi gani atakavyoviondosha au atakavyovipa majina mapya, ili tutakapokuja kwenye bajeti inayokuja au katika kitabu chetu kipya, basi angalu kuwe na maelekezo mazuri zaidi kuliko haya ambao tuliyokuwa nayo. Hilo tutalifanyia kazi.

Umetoa pendekezo kwamba tuwe na kitabu kimoja tu cha bajeti badala ya kuwa na vitabu vingi vya bajeti. Mimi ninasema, tutayachukua na tutayajadili. Mimi ningependa zaidi kila wizara ingekuwa na kitabu chake. Maana yake ingekuwa ni wepesi wa kukifanyia kazi lakini kutokana na hali ya kifedha. Nadhani Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa umekwenda huko kutokana na hali ya kifedha, kama katika kuhakikisha kwamba matumizi mazuri basi tuwe na kitabu kimoja. Tutaliangalia jinsi gani vipi ipo *effective*, kwa maana ya utekelezaji, *effective* kwa maana ya kifedha. Tutaona kwamba nini tufanye lakini wazo lako tumelipokea na sio baya.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad tumepokea pongezi na umeeleza kwamba matumizi mazuri. Nimeeleza kwa ujumla tutayasimamia kwa mujibu wa vifungu vilivyoekwa hapo. Lakini vile vile ninataka nisisitize kwa Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, uhaulishaji unaanza ndani ya wizara yake. Wizara yake inampelekea Waziri, Waziri anasaini.

Nitawaomba Mawaziri wenzangu angalieni vifungu munavyoletewa ambavyo vinavyotakiwa kuhaulishwa, ulizeni zile hoja ambazo zimeletwa ndani ya Baraza la Wawakilishi hazipo tena kabla hujasaini. Mimi akiniletea Waziri mwenzangu kishasaini, nitashindwa kuanza kuhoji wakati yeye kule hakuhoji. Kwa hivyo, na mimi nitasaini. Hapa tutakuwa hatutekelezi yale maombi ambayo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wameyataka. Tutumie kwa mujibu wa maidhinisho ya vifungu. (*Makofi*)

Hivyo, na mimi nitawaomba sana Mawaziri wenzangu tusitie saini tu, tusomeni vile vifungu ambavyo vilivyohaulishwa kwa madhumuni gani wanataka wenzetu kuvihaulisha. Tumepokea Mhe. Mohammed Mbwana Hamad.

Mhe. Mohammed Haji Khalid kuhusu watendaji kuwa waadilifu. Ninadhani serikali nzima tupo hapa, tutalisimamia hilo. Kila Waziri, kila Katibu Mkuu tutalisimamia hilo tukiongozwa na Makamu wa Pili wa Rais na ndilo jukumu letu. Bila ya kuwa na watendaji waadilifu, serikali nzima nayo itakuwa haina uadilifu. Ni lazima tuwe na watendaji waadilifu tuweze kuanzia hapo.

Umetaka fedha za maendeleo ni chache lakini tuweze kuzitumia kwa maendeleo. Tunakubali ili tuweze kuendelea kwa haraka lazima tuwekeze zaidi katika miundombinu. Kwa hivyo, ndio fedha zetu za maendeleo. Hili tumelipokea na tutalisimamia, nikishirikiana na Mawaziri wenzangu kwa sababu kila Waziri ana miradi ya maendeleo ndani ya wizara yake.

Mhe. Spika, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk ambaye ni shemegi yangu. Sheria hizi zote za fedha zinamlinda Waziri wa Fedha. Akitekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, ninarudia sheria za fedha pamoja na hii sheria ambayo ya kuidhinisha matumizi, pamoja na sheria ya *Financial Bill*, zote zinamlinda Waziri wa Fedha lakini akitekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria, akitekeleza majukumu yake nje ya sheria, sheria hizo zitakuwa hazimlindi. (*Makofi*)

Mimi ninataka nitekeleze majukumu yangu kwa mujibu wa sheria. Mhe. Spika, na ninamuomba sana Mwenyezi Mungu anisaidie nitekeleze majukumu yangu kwa mujibu wa sheria, ili sheria hizi ziweze kunilinda.

La pili ambalo Mhe. Makame Mshimba Mbarouk umetutaka kwamba wale ambao wanaodai basi walipwe. Na mimi ninawaambiwa Mawaziri wenzangu wawambie Makatibu Wakuu, kwa wale ambao wanaotudai ndani ya mawizara yetu, basi tukipata hicho hicho kidogo, tuanzishe utaratibu wa kulipa kidogo kidogo ili tuondokane na haya madeni. Kwa sababu madeni munakaa nayo muda mrefu, nyinyi pesa munapata munatumia hamlipi. (*Makofi*).

Mhe. Spika, nitatoa mfano mzuri. Natoa mfano mmoja mzuri sana, Shirika la Umeme *(ZECO). ZECO* anawadai mawizara katibu yote haya na kila wizara hapa inapitisha kifungu cha kulipa umeme, lakini wanapopewa ile *OC* hawaweki pesa za kulipa umeme. Hivi sasa tumebeba lile jukumu tunamlipa *ZECO* kupitia mfuko mkuu wa Hazina. (*Makofi*)

Sasa mimi ninataka niwaambie wenzangu Mawaziri wenzangu na ninataka nisisitize hapa kwamba *ZECO* na wao waweke *TUKUZA* ndani ya mawizara. Kama Waziri atakuwa hawezi kusimamia ulipaji wa umeme ndani ya wizara yake, umeme utakuwa hakuna tu, halafu atakumbuka kulipa. Kwa hivyo, kuna majukumu haya ya kulipa madeni jamani, lazima tuwe na utamaduni wa kulipa, tusiwe na utamaduni tu wa kukopa na kutuma. Kwa hivyo, hili wenzangu wamenisikia. (*Makofi*)

Mhe. Ali Mzee Ali, *professor* huyu. Ninakushukuru sana kwa pongezi. Umeeleza historia ni kweli *for the first time*, ukitizama historia ya nyuma, bajeti yetu tunazungumza mpaka Julai kumi na tano au Julai thalathini. Ndio tunakuja kusoma *Approbation Bill*. Leo tarehe ishirini na nane Mhe. Spika, jana ilikuwa ni *birdhday* yangu lakini hujanipa *happy birthday*. Kwa hivyo, ninajitangazia mwenyewe, jana nilikuwa ni *birthday. (Makofi*)

Mhe. Spika, leo ni tarehe ishirini na nane tunapitisha sheria ya *Approbation Bill*. Ndio hili analolisema *professor* Mhe. Ali Mzee Ali. Huo *professor* amepewa na Waziri wa Elimu aliyekuwepo Mhe. Haroun Ali Suleiman, sio mimi, mimi ninaendeleza tu. Ndio anasema kuwa hii ni historia. Tukifika tarehe moja keshokutwa tumeshapitisha mpaka *Approbation Bill*, tunaanza tuko safi kabisa, hatuna matatizo. (*Makofi*)

Ndio kwa maana akasema kuwa hii ni historia na inapaswa kupongezwa chini ya jemedari mkuu wetu Dkt. Ali Mohammed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mimi sikuliona hili na ndio kwa maana huyu amepewa jina la u-*professor* ameliona. Tunakushukuru bwana sana. *(Makofi)*

Amenipa pongezi nyingi sana. Nimezipokea lakini mimi ninataka nizirudishe pongezi hizi kwa wale ambao wamenilea. Nikianza kwanza na Mhe. Ali Juma Shamuhuna ambaye amenilea. Amenilea huyu miaka saba. Waziri wangu wa Mipango miaka mitano na Afisi ya Waziri Kiongozi miaka miwili, miaka saba amenilea Mhe. Ali Juma Shamuhuna. (*Makofi*)

Amenilea vile vile marehemu Mhe. Salum Juma Othman alikuwa waziri wangu pia, amenilea vile vile Mhe. Prof. Juma Kapuya. Alikuwa ni Waziri wangu kwenye Wizara ya Ulinzi na vile vile amenilea Mhe. Mustapha Mkulo, alikuwa ni Waziri wangu kwenye Wizara ya Fedha. (*Makofi*).

Hata hivyo aliyenilea vizuri zaidi miaka minne hii ya mwanzo, ni Dkt. Ali Mohammed Shein - Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Huyu amenilea miaka mitatu na nusu ya mwanzo. Mimi sikujua kama Rais huwa anachungulia chungulia na kutazama. Mwezi wa nane ninakumbuka niliikuwa nipo likizo Kuala Lumpur, nje ya nchi.

Katibu Mkuu wangu akaniletea *message* hongera. Rais sasa ametuachia, tupo wenyewe. Nikasema hii kazi kubwa sana sasa! Maana yake unapokuwa na mzazi, kila siku unajua kwamba mzazi yupo, hata ukikosea mzazi yupo. Sasa tupo peke yetu!

Niliporejea nilimwita Katibu Mkuu wangu nikamwambia sasa tuongeze nguvu zaidi ya kufanya kazi ili Mhe. Rais yale mategemeo yake ya kutuachia ayaone kwamba yana matunda. Ninamshukuru sana Mhe. Rais, ameona utendaji wetu mimi na wenzangu ndani ya wizara na sasa tunatekeleza majukumu yetu. Tutaendelea kutekeleza majukumu yetu kwa dhati Mhe. Spika, ili hatimaye wananchi wa Zanzibar waweze kufaidika na matunda ya serikali yao. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwenye bajeti inayokuja Mhe. Ali Mzee Ali umetaka tuoneshe mabadiliko. Tutajitahidi na tuoneshe nguvu zetu zote tuoneshe mabadiliko. Tusimamie bei za vitu katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani, nimeeleza, tutasimamia kwa nguvu zetu zote na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko tumeshaandaa mkakati wa kusimamia. (*Makofi*)

Sasa Mhe. Spika, ninakuja kwa Mhe. Mgeni Hassan Juma. Umeeleza suala la kusimamia matumizi na uvujaji nimeshalitolea maelezo. Vile vile umeeleza kwamba fedha zinazoingia katika asasi za kiraia nyengine hazionekani zinakwenda kufanya shughuli gani. Tutalifanyia kazi kwa nguvu zetu zote ili tuweze kuelewa hasa kila kinachoingia na kinachotekelezwa kwa faida ya wananchi wa Zanzibar.

Umenitaka vile vile fedha zinazokuja kwa jina la Tanzania tuweze kuona na sisi Zanzibar tunafaidika vipi. Tumeshaanza kufanya mazungumzo baina ya Wizara zetu mbili za Fedha. Mhe. Waziri wa Fedha wa Muungano Mhe. Saada Mkuya ameona hiyo hoja na sasa tunalifanyia kazi kwa pamoja zaidi.

Umetaka ujue taarifa kuhusu *Obama Initiatives*. Nasema zikishakuwa tayari tutakuja kutoa taarifa ndani ya Baraza lako Tukufu Mhe. Spika.

Mhe. Fatma Mbarouk Said umezungumzia juu ya mikataba inayokatibiwa baina yetu sisi serikali na taasisi nyengine, iwe mizuri na isiwe ya kupoteza mapato ya serikali au fedha za serikali. Serikali imetoa muongozo kuwa mikataba yote sasa hivi ni lazima ipitishwe kwa Mwanasheria Mkuu na Mwanasheria Mkuu aipitie na aikubali kwamba hii mikataba sasa inaweza ikafanyiwa kazi.

Ninataka nimshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu kwa kweli amekuwa akichukua jukumu hilo na mikataba hii ambayo nimekuwa karibu mimi niliyokuwa nimeiona, hasa ile inayohusiana na afisi yangu, kwa kweli ameweza kutusaidia. Nitamuomba sana aendelee kufanya hivyo.

Mheshimiwa umetaka nikupe ufafanuzi juu ya kifungu namba 5 (1). Nimeruhusiwa kukopa kwa matumizi na katika muda wa Juni 30. Mkopo ndio mkopo, unaweza ukaupata kwa ukamilifu katika mwaka ule na unaweza ukaupata kutegemeana na matumizi. Wenzetu wengi unaowakopa wanakupa pesa kwa mujibu unavyowafanyia kazi.

Ukionekana kwamba kazi ile imechelewa na wao mkopo utachelewa kutoka. Tutajitahidi sana kusimamia ili kile tunachokikopa ndani ya mwaka huu, basi tuweze kukipata ndani ya mwaka huu kwa matumizi yetu. Umetaka nikutolee ufafanuzi juu ya ile bilioni ishirini na mbili. Zile ni fedha ambazo zipo ndani ya bajeti yetu hivi sasa, ambazo tunapaswa kuzitumia kulipia mikopo na riba. Kiwango kile tu Waziri wa Fedha amepewa dhamana, kiwango kile tu hatakiwi kutumia zaidi, mikopo na riba tutumie *22 billions* basi.

Mhe. Marina Joel Thomas umezungumzia juu ya usimamizi mzuri. Kama nilivyosema tutasimamia kwa nguvu zetu zote. Lakini ninawaomba vile vile Waheshimiwa Wajumbe Mhe. Spika, watusaidie katika usimamizi. Tuna Kamati ya *PAC*, hii ina jicho la ndani zaidi na wao vile vile watusaidie pamoja na kamati nyengine watakapokuwa wanatembelea katika wizara zetu.

Udhibiti na uvujaji wa mapato; nalo vile vile nimelitolea ufafanuzi na ninataka nilihakikishie Baraza lako Tukufu kwamba tutajitahidi kuona kwamba mapato yetu yasivuje kiasi ambacho kinachoonekana kwa sasa.

Fedha za mikopo zisimamiwe ili zitumike vizuri. Hilo ndio lengo. Lengo la serikali na lengo la mkopeshaji. Mkopeshaji anapoona kwamba fedha za mikopo umezitumia vyenginevyo, anasitisha mikopo yake. Kwa sababu ni lazima tupeleke ili tuweze kuidhinishiwa matumizi mengineyo. Kwa sababu hupewi zote kwa mpigo, unapewa kila baada ya utekelezaji na wewe unatakiwa utoe *certificate* kwamba hapa nimeshatelelezeka naomba sasa fedha nyengine. Yeye anaangalia kweli umetekeleza lile tuliyoyalibaliana.

Fedha ziingizwe katika vifungu vya mawizara kwa wakati. Tutajitahidi Mhe. Marina Joel Thomas kulingana na hali ya makusanyo tutajitahidi, lakini kama nilivyosema matumizi ni makubwa ukilinganisha na mapato, lakini tutajitahidi pale inapobidi basi tuingize fedha hizo kwa wakati.

Mhe. Spika, baada ya kutoa ufafanuzi kwa hoja zote hizo, kwa heshima na taadhima, sasa basi naomba kwa ruhusa yako kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

MSWADA WA SHERIA YA MAKISIO YA MWAKA 2014

Kifungu 1 Jina Fupi
Kifungu 2 Tafsiri
Kifungu 3 Utoaji wa Shilingi 707,829,640,000/- kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali
Kifungu 4 Makisio ya Fedha Zilizokubalika
Kifungu 5 Uwezo wa Waziri Kukopa
Kifungu 6 Uwezo wa Waziri wa Maombi ya Ziada
Kifungu 7 Marejesho ya Mkopo na Riba
Kifungu 8 Kukubaliwa kwa Mipango ya Maendeleo
Kifungu 9 Kukubaliwa kwa Fedha Zilizopitishwa kwa Matumizi ya Maendeleo

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia mswada wangu kifungu kwa kifungu na kuukubali bila ya marekebisho. Sasa naliomba Baraza lako Tukufu liukubali, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri. Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na mswada huu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Makisio ya Mwaka 2014)

(Kusomwa kwa Mara ya Tatu)

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kwamba Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Bilioni Mia Saba na Saba, Mia Nane na Ishirini na Tisa Milioni, Mia Sita na Arobaini Elfu (707,829,640000) kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia siku ya tarehe 30 Juni, 2015 na kuruhusu utoaji na uhaulishaji wa fedha hizo pamoja na mambo yanayohusiana na hayo, usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Sasa niwahoji Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na mswada huu katika kusomwa mara ya tatu wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Mswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa
Mara ya Tatu na Kupitishwa)

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria wa Maadili ya Viongozi wa Umma Zanzibar, 2014

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kusoma kwa mara ya kwanza Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Kuanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi na Mambo yanayohusiana na Hayo. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mswada umeshasomwa kwa mara ya kwanza na uko tayari kufanyiwa kazi na Kamati inayohusika. *(Makofi)*

Sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria.

Mswada wa Sheria ya Wauguzi na Wakunga, 2014

(Kusomwa kwa Mara ya Kwanza)

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kusoma kwa mara ya kwanza Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Wauguzi na Wakunga na Uanzishwaji wa Baraza la Usajili la Wauguzi na Wakunga nam. 9 mwaka 1986 na Kuanzisha Sheria mpya ya Wauguzi na Wakunga na mambo yanayohusiana na hayo. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mswada umeshasomwa kwa mara ya kwanza na sasa uko tayari kufanyiwa kazi na Kamati inayohusika. *(Makofi)*

KAULI ZA SERIKALI

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA HAKI NA USTAWI WA WATOTO KWA MWAKA 2013/2014

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya njema na kutuwezesha kukutana hapa tukiwa wazima.

Vile vile napenda kuchukua fursa hii kukushukuru wewe Mhe. Spika pamoja na Wajumbe wa Baraza lako Tukufu la Wawakilishi, kwa kuniruhusu kuwasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Haki za Watoto kwa mwaka 2013/2014.

Mhe. Spika, tarehe 16 Juni ni siku ya Maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, ambayo huadhimishwa kila mwaka na nchi zote wanachama wa Umoja wa Afrika, kwa madhumuni ya kuwakumbuka watoto waliouawa kikatili mwaka 1976 mjini Soweto Afrika ya Kusini, wakipinga ubaguzi na utumiaji wa lugha ya Kikaburu maskulini.

Mhe. Spika, siku hii inatoa fursa kwetu kupima utekelezaji wa haki za watoto na kupendekeza hatua madhubuti za kuchukuliwa kwa nia ya kuimarisha huduma zinazolenga watoto. Pia inatupa msukumo wa kuzidisha mashirikiano

baina ya wazazi, walezi, sekta zinazohudumia mama na mtoto pamoja na washirika wa maendeleo kwa utekelezaji wa Sheria ya Mtoto ya mwaka 2011.

Ujumbe wa Siku ya Mtoto wa Afrika kwa mwaka 2014 ni *"Elimu Bora Isiyo na Vikwazo ni Haki ya Kila Mtoto"*. Mhe. Spika, ujumbe huu pamoja na mambo mengine una madhumuni yafuatayo:-

1. Kujenga mazingira kwa mtoto ya kupata elimu bora isiyo na vikwazo;

2. Kuhakikisha upatikanaji wa mahitaji muhimu pamoja na kushughulikia masuala ya kiutamaduni na kijamii yanayoweza kuathiri maendeleo ya elimu kwa mtoto;

3. Kusaidia kujenga uelewa juu ya umuhimu wa elimu na kuwashirikisha watoto katika masuala yao; na

4. Kukuza mashirikiano miongoni mwa wahusika mbali mbali, ili kuongeza fursa za upatikanaji wa haki ya elimu kwa watoto.

Kwa kweli, ujumbe huu una maana kubwa kwetu kwani unahimiza tuchukue hatua za makusudi za kuhakikisha kwamba watoto wetu wanapata elimu iliyo bora na itakayowaandaa vyema kukabiliana na mazingira wanayoishi.

Utekelezaji kwa Mwaka 2013/2014

Mhe. Spika, Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto, ambayo inaratibu na kusimamia shughuli za maendeleo ya watoto Zanzibar, imeandaa utaratibu wa kuwasilisha mbele ya Baraza lako Tukufu taarifa za kila mwaka za utekelezaji wa haki za mtoto ifikapo tarehe 16 Juni ya kila mwaka.

Taarifa hii ya utekelezaji wa haki za watoto kwa mwaka 2013/2014 inajumuisha sekta zote za serikali na zisizo za kiserikali zinazoshughulikia masuala ya watoto kulingana na mikataba, malengo ya *millennium*, sera na mipango ya kitaifa ya maendeleo, MKUZA II 2010/2015 na Dira ya 2020.

Mhe. Spika, wizara imeandaa mkakati wa kisheria wa haki za watoto wenye lengo la kuhakikisha kuwa utekelezaji wa masuala ya sheria unazingatia haki za watoto na unaendana na mikataba ya Kimataifa, Sheria ya Mtoto nam. 6 ya mwaka 2011. Mkakati huo una maeneo saba yafuatayo yanayofanyiwa kazi:-

- Kuongeza ufahamu kwa watoto na jamii juu ya haki za watoto;
- Kuongeza uwezo wa taasisi zinazoshughulikia masuala ya sheria na mifumo ya kutoa haki nchini, ili iweze kushughulikia watoto wanaokinzana na sheria kwa mujibu wa viwango vya kimataifa;
- Kuimarisha mfumo wa kushughulikia watoto wanaotoa ushahidi katika kesi za wanaoathirika kutokana na kunyimwa haki zao;
- Kuimarisha utekelezaji wa masuala ya hifadhi ya mtoto;
- Kuongeza ufikiwaji wa huduma za msaada wa kisheria kwa watoto watakaohitaji huduma hizo; na
- Kuweka mfumo wa uhakika wa ufuatiliaji na uratibu wa masuala ya sheria kwa watoto.

Mhe. Spika, mafanikio yamepatikana katika kumlinda mtoto kwa kuanzisha Mahkama ya Watoto Vuga pamoja na kufungua Dawati la Ziada la Jinsia na Watoto katika Kituo cha Polisi Mwera. Hali hii inafanya jumla ya Madawati nane, manne Unguja na manne Pemba. Sehemu ambazo madawati hayo yameanzishwa katika vituo vya Polisi kama vile Madema, Mwera, Makunduchi na Mfenesini kwa upande wa Unguja, vyengine ni Madungu, Mkoani, Wete na Micheweni kwa upande wa Pemba.

Mhe. Spika udhalilishaji wa watoto bado ni tatizo katika jamii yetu. Taarifa juu ya matukio ya udhalilishaji ni kama ilivyoelezwa kwenye Taarifa ya Utekelezaji wa Haki za Watoto kwa mwaka 2013/2014.

Mhe. Spika, makuzi ya mtoto yanahitaji matunzo na huduma muhimu, ili mtoto aweze kukua kiafya, kimwili na kiakili. Serikali imeendelea kuwatunza Watoto Yatima katika Nyumba ya Watoto Mazizini na kuwapatia huduma zote zinazostahili. Aidha imeendelea kutoa huduma za msaada wa kujikimu kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu, jumla ya familia 132 zinanufaika na huduma hizi katika maeneo mbali mbali kama ilivyoainishwa katika taarifa ya utekelezaji.

Mhe. Spika, haki ya kushiriki na kushirikishwa inatoa fursa na uhuru kwa watoto kushiriki na kujadili katika masuala yanayowahusu. Kupitia Mabaraza yao watoto wamepata fursa ya kutoa maoni yao juu ya masuala mbali mbali ya kitaifa yaliyojitokeza ikiwemo suala la udhalilishaji. Hivyo, nachukua fursa hii kutoa pongezi kwa Mabaraza yote ya Watoto kwa namna wanavyopiga vita utoro maskulini, kupinga udhalilishaji na kuhimiza kuhusu maadili mema.

Vile vile, suala la ukuaji na maendeleo ya mtoto unategemea afya bora ikiwemo lishe, kukingwa dhidi ya maradhi na mazingira bora ya kiafya kabla na baada ya kuzaliwa. Wizara ya Afya imeweza kununua chanjo na kutoa chanjo zaidi ya asilimia 98 ya watoto wamepatiwa chanjo dhidi ya maradhi mbali mbali kwa Unguja na Pemba. *(Makofi)*

Katika jitihada za kuzuia maambukizi mapya ya UKIMWI miongoni mwa watoto, jumla ya watoto 228 waliozaliwa na mama wanaoishi na VVU wamepewa dawa ya kinga dhidi ya maambukizi hayo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, maji safi na salama ni muhimu sana katika uhai wa mtoto. Katika kuimarisha upatikanaji wa maji safi na salama miradi 30 ya uchimbaji wa visima, ujenzi wa matangi, usambazaji wa mabomba pamoja na uwekaji wa miundombinu imekamilika kwa baadhi ya maeneo, ikiwemo Nungwi, Kilombero, Pete, Kokota, Mkwajuni, Matemwe, Chwaka, Kojani, Michenzani, Umbuji, Kilindi, Ziwani na Kiwani. *(Makofi)*

Aidha, katika kuimarisha usafi wa mazingira jumla ya skuli 80 za Unguja na Pemba zinafaidika na huduma za ujenzi wa vyoo. Mhe. Spika, watoto kama hazina ya Taifa wanahitaji kuendelezwa kielimu. Katika mwaka 2013/2014 jumla ya watoto 22,134 wameandikishwa katika skuli za maandalizi 457 kwa Unguja na Pemba, kati ya hao wanaume ni 11,049 na wanawake ni 11,135. Kwa upande wa elimu ya msingi jumla ya wanafunzi wapya 252,938 wameandikishwa Unguja na Pemba, kati ya hao 126,988 ni wanawake na 125,950 ni wanaume.

Mhe. Spika, serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mashirikiano na wananchi pamoja na washirika wa maendeleo imekuwa ikiongeza idadi ya madarasa na skuli kwa lengo la kutanua huduma za elimu, serikali imekamilisha ujenzi wa skuli mpya 13 na tayari zimeanza kutumika.

Katika kuhakikisha kuwa vijana wanapata taaluma ya stadi mbali mbali, jumla ya wanafunzi 49 wakiwemo wanaume 35 na wanawake 14 wamepatiwa mafunzo katika fani ya umeme, uchongaji na utunzaji nyumba na wamemaliza masomo yao katika mwaka 2013/2014 katika Kituo cha Elimu Mbadala.

Aidha serikali pia inaendeleza juhudi za upatikanaji wa vifaa vya kusomea na kufundishia, ili kuweka mazingira mazuri ya kufundisha na kusoma katika maskuli.

Mhe. Spika, ili kuhakikisha kwamba watoto wenye ulemavu wanashiriki na kupata haki zao za msingi za elimu kama inavyoelekezwa na mikataba ya kikanda na kimataifa pamoja na sera za kitaifa. Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Maendeleo ya Watu Wenye Ulemavu imeweza kushajihisha na kuhamasisha wanajamii juu ya umuhimu wa elimu kwa watoto wote, jumla ya watoto wenye ulemavu 1,601, kati ya hao wanawake 657 na wanaume 944 waliandikishwa skuli Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, upatikanaji wa habari na michezo ni msingi wa maendeleo kwa watoto, jumla ya vipindi 2,409 vya televisheni na 56 vya redio vinavyohusu masuala ya watoto vimerushwa hewani kwa kushirikiana na Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*). Aidha makala mbali mbali zinazohusu masuala ya watoto zimetolewa kupitia Gazeti la Zanzibar Leo.

Mapambano dhidi ya ajira mbaya za watoto yanaendelezwa. Jumla ya watoto 3,600 wenye umri chini ya miaka 15 waliokuwa katika ajira za watoto na ambao wako kwenye hatari ya kuingia katika ajira hizo kwenye shehia 16; kwa Unguja ni shehia 8 na Pemba 8 wamerejeshwa skuli.

Vile vile, kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto nam. 6 mwaka 2011 mtoto anayo haki ya kusajiliwa mara tu anapozaliwa. Hadi kufikia mwezi wa Februari, 2014 Ofisi ya Mrajis wa Vizazi na Vifo imesajili jumla ya watoto 36,826, kati ya hao wanawake ni 18,303 na wanaume 18,523. Aidha jumla ya vifo vya watoto 2,228 vilisajiliwa Unguja na Pemba, ambapo kati ya hivyo 1,200 ni vya watoto wa kiume na 1,028 ni vya watoto wa kike.

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana bado kuna changamoto kadhaa katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo katika sekta mbali mbali, ikiwemo mimba za utotoni, watoto kuolewa mapema pamoja na utoro ni miongoni mwa changamoto zinazokwaza maendeleo ya elimu kwa watoto hasa wa kike.
Aidha vitendo vya udhalilishaji vinaendelea kutokea kila leo pamoja na juhudi kubwa ya serikali na washirika katika kupambana na tatizo hilo.

Hivyo, naomba kutoa wito Mhe. Spika, kwa wakuu wa wizara, idara na taasisi nyengine mbali mbali za serikali na zisizo za kiserikali pamoja na sekta binafsi watoe kipaumbele masuala ya maendeleo ya watoto katika mipango na bajeti zao, aidha naomba kuikumbusha jamii, watendaji na viongozi kwamba sote tuna wajibu sawa kwa kusimamia watoto wetu na kukemea yale yote yanayowadhalilisha watoto kwa kukosesha haki zao pamoja kuchukua hatua madhubuti kukabiliana na ukiukwaji wa haki za watoto.

Mhe. Spika, natoa shukurani za dhati kwa taasisi zote za Serikali zilizoshiriki katika uandaaji wa taarifa hii, aidha natoa shukurani kwa washirika wa maendeleo ikiwemo *UNICEF* na *Save the Children* ambao wamekuwa wakisaidia juhudi za Serikali za kuimarisha ustawi na upatikanaji wa haki za mtoto. Pia natoa shukurani kwa taasisi zisizo za Kiserikali ambazo zimekuwa mstari wa mbele katika kusimamia masuala ya watoto ikiwemo *ZAFELA, ZAPHA+* , *ZACA* na Bodi ya ushauri ya watoto Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa heshima na taadhima naomba kuwasilisha.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Mhe. Spika, Kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii naomba kusoma Ripoti ya Kamati kuhusiana na utekelezaji wa haki na Ustawi wa Watoto kwa mwaka 2013/2014 na maadhimisho ya siku ya Mtoto wa Afrika yanayofanyika kila mwaka ifikapo tarehe 16 napenda kuisoma mbele yako.

Mhe. Spika, kila sifa njema zinamstahikia Mwenyezi Mungu aliyetujaalia afya na uzima na kutuwezesha Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kuendelea kutekeleza majukumu tuliyokabidhiwa; kwa niaba ya wananchi tunaowawakilisha kupitia nafasi mbali mbali katika Baraza lako Tukufu.

Mhe. Spika, Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwako, kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, kuhusiana na Taarifa ya Utekelezaji wa Haki na Ustawi wa Watoto kwa mwaka 2013/2014 iliyowasilishwa na Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa jamii, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Spika, Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, inaunga mkono taarifa iliyowasilishwa na Mhe. Waziri, ambayo ilikusanya mambo muhimu yanayoelekeza katika kuendeleza ustawi na upatikanaji wa haki za watoto. Pia inayoonesha namna gani nchi yetu inavyochukua jitihada kupitia Wizara zake mbali mbali katika kuyafanyia kazi mapendekezo na maazimio yaliyotolewa na Umoja wa Mataifa, Umoja wa Afrika n.k ili kuhakikisha kuwa, utekelezaji wa mipango ya Wizara hizo inazingatia maazimio hayo kwa lengo la kuleta ustawi na upatikanaji wa haki za watoto katika nchi yetu.

Mhe. Spika, licha ya Kamati yangu kuunga mkono taarifa iliyowasilishwa na Mhe.Waziri lakini Kamati imegundua kuwa, katika taarifa hiyo kumekosekana uwasilishwaji wa taarifa ya utekelezaji kwa mwaka uliopita wa 2012/2013 ambapo imekuwa ni vigumu kwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, wasikilizaji au wasomaji wengine wa taarifa hiyo, kuweza kufahamu na kulingalisha hatua zilizofikiwa za utekelezaji wa haki na ustawi kwa mwaka uliopita na muelekeo kwa mwaka unaokuja. Hivyo Kamati inaishauri Wizara, pindi itakapokuwa inawasilisha taarifa ya

utekelezaji katika Baraza lako Tukufu, ni vyema ikazingatia kuingiza taarifa ya utekelezaji wa mwaka uliopita ili iwe rahisi kwa Wajumbe wa Baraza, wasikilizaji na wasomaji wengine kuweza kulinganisha hatua zilizofikiwa za utekelezaji wa haki na ustawi wa watoto.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi napenda kuchukua fursa hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati pamoja na makatibu wake kama hivi ifuatavyo:-

1. Mhe. Mgeni Hassan Juma Mwenyekiti
2. Mhe. Hassan Hamad Omar M/Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Salum Haji Mjumbe
4. Mhe. Abdi Mosi Kombo Mjumbe
5. Mhe. Farida Amour Mohamed Mjumbe
6. Mhe. Mwanaid Kassim Mussa Mjumbe
7. Mhe. Mohamed Mbwana Hamad Mjumbe
8. Ndg. Maryam Rashid Ali Katibu
9. Ndg. Asha Said Mohamed Katibu

Mhe. Spika, siku ya Mtoto wa Afrika ni siku muhimu ambayo inaadhimishwa kila mwaka ifikapo tarehe 16 Juni, na katika siku hii, jamii inapata fursa ya kufahamu hatua zilizofikiwa na Wizara katika kutekeleza haki za watoto na hatua zilizopendekezwa kuchukuliwa kwa nia ya kuimarisha huduma zinazolenga watoto pamoja na kuimarisha mashirikiano baina ya wazazi, walezi, sekta zinazohudumia mama na mtoto pamoja na washirika wa maendeleo.

Mhe. Spika, maoni ya Kamati yangu yatagusa maeneo mbali mbali yanayohusiana na Wizara hii ikiwa ni pamoja na baadhi ya maeneo ya taarifa iliyowasilishwa na Mhe. Waziri na Kamati itatoa ushauri kwa Serikali, Wizara na Jamii kwa ujumla.

KUHUSU KINGA DHIDI YA VITENDO VYA UDHALILISHAJI WA WATOTO

Itakumbukwa kuwa, katika kikao cha Disemba cha 2013, Mhe Mwenyekiti wa Kamati hii, Mgeni Hassan Juma aliwasilisha hoja binafsi inayohusiana na kutoa Maazimio Dhidi ya Vitendo vya Udhalilishaji wa Watoto na Wanawake Zanzibar, ambapo hoja hiyo ilitolewa kwa mujibu wa Kanuni ya 27(1)(n), 27(3), 49(1) na Kanuni ya 50 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2012.

Mhe. Spika, katika hoja hiyo kulikuwa kuna mambo ya msingi ambayo yalihitaji kushughulikiwa kwa haraka, na miongoni mwa mambo hayo ni kuitaka Serikali kuanzisha mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na kutokomeza udhalilishaji wa watoto; utakaojumuisha wawakilishi kutoka makundi mbali mbali, na pia kulikuwa na azimio la kuitaka Serikali kuweka kipaumbele katika bajeti zake kuanzia bajeti ya mwaka 2014/15 na bajeti zinazofuata, juu ya suala la kupambana na kutokomeza udhalilishaji wa watoto.

Mhe. Spika, jambo la kusikitisha ni kwamba, hadi hivi ninapowasilisha hotuba hii, Serikali haijatoa tamko lolote kuhusiana na maazimio yaliyotolewa na Baraza katika hoja hiyo muhimu, yenye dhamira ya kuwalinda watoto na wanawake dhidi ya udhalilishaji, Hivyo Kamati inaitaka Serikali kutoa tamko juu ya hatua zilizofikiwa katika hoja hiyo.

KUHUSU MALALAMIKO YA VITENDO VYA UDHALILISHAJI WA WATOTO NA NAMNA KESI ZINAVYOSHUGHULIKIWA.

Kamati imekuwa ikishuhudia jitihada mbali mbali zinazochukuliwa na Wizara hii, katika kupinga vitendo vya udhalilishaji wa watoto kama vile kuanzishwa kwa Vituo vya Mkono kwa Mkono Unguja na Pemba na Kamati za

Shehia za Kupinga vitendo vya udhalilishaji. Kamati inaipongeza Wizara na inaziunga mkono jitihada hizo, lakini kwa upande mwengine Kamati yangu imekuwa inasikitishwa sana na uchache wa kesi zinazohukumiwa.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Julai 2013 hadi Machi 2014, jumla ya malalamiko 2,337 (Unguja 2,239 na Pemba 98) yameripotiwa katika vituo vya Mkono kwa Mkono lakini katika malalamiko hayo, 87 tu ndio yaliyowasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka.

Kamati imebaini kuwa idadi hiyo ni ndogo sana ukilinganisha na malalamiko yaliyoripotiwa ambapo waathirika wakubwa ni watoto wenye ulemavu hasa hasa wenye ulemavu wa akili. Hivyo Kamati inaiomba Serikali kuangalia kuna matatizo gani yanayopelekea hali hiyo na kuchukua hatua za haraka katika kuyatafutia ufumbuzi malalamiko ya kesi zilizoshindwa kushughulikiwa. Kufanya hivyo kutapelekea watoto kupatiwa haki yao ya kuishi na kuhifadhiwa kutokana na vitendo vya udhalilishaji.

KUHUSU MISAADA NA USTAWI WA WATOTO

Kamati inaipongeza Wizara kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii, kufanya zoezi la utambuzi wa watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi katika Wilaya 5 za Unguja (Mjini, Kati, Kusini, Kaskazini A na Kaskazini B) na Wilaya 3 za Pemba (Mkoani, Chake Chake na Micheweni) na kubaini kuwa, kuna watoto wapatao 698 (332 wanawake na 366 wanaume) wanaoishi katika mazingira magumu zaidi.

Mhe. Spika, kamati yangu inatambua kuwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi wanahitaji kusaidiwa, lakini ukweli ni kuwa, Wizara haijatengewa bajeti maalum na ya kutosha kwa ajili ya kuwahudumia watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi. Hivyo Kamati inatoa wito kwa Serikali kutenga bajeti maalum kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi, kuzingatia masuala ya watoto katika mipango na bajeti na pia kuitaka jamii kuchukua jukumu la kuwahudumia watoto wao na kusaidia familia ambazo zinaishi katika mazingira magumu kwa wale wenye uwezo wa kufanya hivyo.

Mhe. Spika, aidha Kamati inaipongeza Serikali kwa utaratibu wa kuwapatia msaada wa shilingi 20,000/= kwa kinamama wanaojifungua watoto mapacha kwani ni jambo jema sana na Kamati inaiomba Serikali kufikiria kuongeza kiwango hicho cha fedha ili kiendane na hali halisi ya maisha, kwani kiukweli kwa hali yetu ya uchumi kiwango cha 20,000 ni kidogo sana katika kukidhi mahitaji ya kinamama hao na watoto wao.

Mhe. Spika, jukumu la kuwatunza na kuwalea watoto ni la kila mmoja wetu, na ninapoyasema haya ni vyema ikafahamika kuwa, kutunza na kulea huko si lazima iwe kwa mtoto uliyemzaa mwenyewe tu, bali ni matunzo ya watoto wa jamii nzima, nikimaanisha pia katika kuwasaidia wototo ambao ni yatima au walioko katika mazingira magumu katika jamii.

Kwa namna ya pekee na kwa dhati kabisa Kamati yangu inaipongeza jumuiya ya *ZOP* (*Zanzibar Outreach Program)* kwa kuwa mstari wa mbele kuwasaidia watoto waliopoteza wazee wao katika ajali ya meli ya *Mv Spice Islander*. Ni vyema Serikali ikaunga mkono juhudi kama hizo ili zisaidie kwa watoto wetu katika kupata haki na fursa sawa, kuishi na kuthaminiwa katika nchi yao.

KUHUSU NYUMBA YA KULELEA WATOTO MAZIZINI

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa na dhamira njema ya kuanzisha nyumba ya kulelea watoto iliyopo Mazizini. Kwa kweli dhamira hii inastahili pongezi, lakini Kamati yangu imekuwa hairidhishwi hata kidogo na hali ya uendeshaji wa nyumba hiyo unaotokana na ufinyu wa bajeti inayotengwa kwa ajili ya kuwahudumia watoto.

Mhe. Spika, kila mmoja wetu anafahamu kwamba, watoto wanahitaji matunzo ya hali ya juu ikiwemo kupatiwa chakula bora, malazi, mavazi na kuwapatia haki zao za msingi ikiwemo kupata elimu. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Idara ya Ustawi wa Jamii ambayo inahusika na utunzaji wa nyumba za kulelea watoto imeombewa kutumia shilingi 291,500,000/= ambazo fedha hizo ni pamoja na kuimarisha hifadhi za wazee, kutoa misaada ya kiustawi kwa wananchi wanaoishi katika mazingira magumu zaidi na kusimamia ulipaji wa fidia kwa watu wanaopatwa na ajali kazini.

Mhe. Spika, ni dhahiri kuwa, bajeti hiyo ni finyu na haiwezi kutosheleza ipasavyo katika kuwahudumia watoto pamoja na kutekeleza shughuli nyengine zilizopangiwa Idara hiyo, hivyo Kamati inashauri Serikali kuongeza bajeti

katika Idara ya Ustawi wa Jamii, ili bajeti ya kuwahudumia watoto nayo ipate kuongezeka na hatimaye nyumba za kulelea watoto ziweze kumudu gharama zao mbali mbali.

KUHUSU MAENDELEO YA ELIMU KWA WATOTO ZANZIBAR

Kamati yangu imekuwa ikishuhudia juhudi za Serikali katika kuwapatia elimu watoto wetu, kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imekuwa ikijitahidi kuboresha elimu ya Maandalizi na kuifanya kuwa ni elimu ya lazima ili kuwapatia watoto msingi bora kabla ya kujiunga na elimu ya Msingi.

Aidha, ni imani ya Kamati yangu kuwa ile program ya *ECD* (*Early Childhood Development*) itaanza kufanya kazi kwa mashirikiano ya wizara tatu zinazohusika ambazo ni pamoja na Wizara ya Elimu, Wizara ya kilimo na Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto ambapo katika *program* hii itajumuisha elimu ya makuzi ya awali ya mtoto; ambayo itajumuisha masuala ya lishe bora katika kumjenga mtoto katika ukuaji wake kiakili na kimaadili, ambao utasaidia ufahamu wa mtoto katika maendeleo yake ya elimu.

Mhe. Spika, aidha katika kuboresha maendeleo ya elimu kwa watoto katika nchi yetu, Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika bajeti ya mwaka 2014/2015 imeazimia kuanzisha mradi wa kuwapatia chakula wanafunzi wa Skuli za maandalizi ambapo mradi utaanzwa kutekelezwa Pemba katika Wilaya ya Kaskazini A. Kamati inaunga mkono azma hii ya Serikali na inachukua fursa hii kuwashajihisha wananchi waliopo karibu na maeneo ya skuli hizo, kuzalisha kwa wingi mazao ambayo yatatumika katika kuwapatia chakula watoto katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na mahindi, mtama, viazi vitamu n.k ili kuunga mkono juhudi za Serikali yetu.

Aidha, Kamati inashauri Wizara ya Afya kuendelea na utaratibu wa kupima afya za wanafunzi maskulini kama vile kichocho, minyoo n.k pamoja na utoaji wa dawa ili kuhakikisha watoto wanakuwa na afya bora.

KUHUSU MAENDELEO YA SEKTA YA AFYA KWA WATOTO ZANZIBAR

Wizara ya Afya ndio yenye dhamana juu ya afya za Wazanzibari, ambapo katika kuhakikisha wanaitekeleza dhamana hiyo, imekuwa ikijitahidi kuimarisha huduma za afya hasa huduma za afya kwa watoto kwa kuwapatia chanjo za kujikinga na maradhi mbali mbali ikiwa ni pamoja na polio, pepo punda, surua n.k.

Aidha katika kuhakikisha kuwa watoto wanapata huduma bora za afya, Serikali kupitia Wizara ya Afya ina mpango wa kujenga wodi mpya ya Watoto katika hospitali ya Mnazi Mmoja. Kamati inaunga mkono juhudi hizo na inashauri kuziboresha zaidi huduma za mama na watoto kwa kuviboresha vituo vya Afya vinavyotoa huduma hizo ili kuhakikisha kuwa inapunguza idadi ya vifo vya watoto wachanga *(Infant Mortality Rate).*

Mhe. Spika, **w**atoto wanaoishi vijijini kwa kiasi kikubwa huwa wanakosa huduma nyingi za Afya kutokana na kutokuwepo kwa miundombinu ya kutosha katika kupeleka huduma hizo ikiwemo miundombinu ya mawasiliano na umeme. Kamati yangu imefurahishwa na utaratibu wa kufikisha huduma za Afya za mikoba katika vijiji vyetu Unguja na Pemba *(Mobile Health Services)* ambapo watoto sasa wamekuwa wakifaidika na huduma mbali mbali za Afya kama vile kupatiwa chanjo, kupatiwa dawa, huduma za matibabu, kupatiwa huduma za lishe n.k ambapo huwasaidia kuondokana na matatizo mbali mbali ya kiafya na kujikinga na magonjwa.

KUHUSU USHIRIKISHWAJI WA WATOTO KATIKA MASUALA MBALI MBALI

Miongoni mwa haki muhimu ya mtoto ni kushirikishwa katika mambo mbali mbali yakiwemo ya kijamii na michezo. Wizara ya Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto kwa muda mrefu sasa imekuwa ikiendelea kuanzisha na kuyaendeleza Mabaraza ya Watoto katika ngazi za Shehia na Wilaya. Hivi sasa kuna mabaraza ya watoto ya Wilaya matatu (3), mawili (2) Unguja na moja (1) Pemba na Mabaraza ya Shehia 218 (Unguja 139 na Pemba 79) ambapo kupitia Mabaraza hayo watoto hupata fursa ya kubadilishana mawazo na kushiriki katika shughuli mbali mbali za kijamii.

Aidha kupitia Mabaraza hayo mafunzo mbali mbali yamekuwa yakitolewa kwa watoto juu ya kufahamu haki zao na jinsi ya kujithamini na kujilinda. Kutokana na umuhimu wa Mabaraza hayo, Kamati inaitaka jamii kuwapa fursa watoto wao katika kujiunga na mabaraza ili waweze kujifunza mambo mbali na kuweza kubadilishana mawazo na uzoefu na watoto wengine.

Mhe. Spika, kwa upande wa ushiriki wa watoto katika michezo, ni jambo la kuzingatiwa na jamii yote kwani michezo ni haki ya watoto na inasaidia katika kumkuza mtoto kimwili, kiakili na kiafya. Hivyo Kamati inatoa wito kwa jamii kuwapa fursa watoto wao katika kupata muda wa kucheza na kushiriki katika michezo ambayo itaendana na mila na desturi zetu.

Aidha Kamati inaishauri Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kupitia vyombo vyake vya habari kuendelea na kubuni vipindi mbali mbali vya watoto ambavyo vitakuwa vinatoa mafunzo zaidi katika kutambua haki zao.

KUHUSU WATOTO WENYE ULEMAVU

Watoto wenye ulemavu wana haki sawa kama watoto wa kawaida na wanahitaji kupatiwa huduma zote za msingi ikiwemo lishe bora, mavazi na makaazi rafiki yatakayowawezesha kufikia huduma mbali mbali wanazozihitaji.

Kamati inaishukuru Serikali kwa kulipa umuhimu suala la kulinda na kutetea haki na fursa sawa kwa watu wenye ulemavu kwa kupitisha Sheria namba 9 ya mwaka 2006, kuanzisha Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu na Idara ya kushughulikia masuala ya watu wenye ulemavu.

Mhe. Spika, pamoja na jitihada zilizochukuliwa na Serikali kwa watu wenye ulemavu, Kamati inaitaka Serikali kupeleka jitihada zake mahsusi ambazo zitawalenga watoto wenye ulemavu moja kwa moja na sio kuwajumuisha na makundi mengine ya watu wenye ulemavu. Kamati inaitaka Serikali kuzitafutia ufumbuzi changamoto zinazowakabili watoto wenye ulemavu kama vile kuwaandalia mazingira rafiki yatayowawezesha watoto hao kufikia huduma muhimu, kuwaandalia walimu wa kutosha na wenye taaluma maskulini na kuwapatia vifaa vya usaidizi kama vile mashine za nukta nundu kwa wasioona ili na wao wapate huduma bora kama zile wanazopatiwa watoto wa kawaida.

Mhe. Spika, kwa kumalizia hotuba hii nachukua nafasi hii kuitaka jamii kwa ujumla kuwatunza, kuwathamini, kuwapenda na kuwalinda watoto wao na kuhakikisha kuwa wanawapa haki zao za msingi ili waje kuwa raia wema katika nchi hii, watakaoweza kuwasaidia wazee wao na nchi yetu. Aidha naomba sote tukumbuke ule usemi usemao "*mtoto umleavyo ndivyo akuavyo*", hivyo nawausia wazazi wenzangu kuwalea watoto wetu katika malezi bora na mema kama maadili na utamaduni wetu unavyotuelekeza.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nachukua tena nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii, kuwasilisha maoni ya Kamati juu ya taarifa ya Utekelezaji wa Haki na Ustawi wa Watoto kwa mwaka 2013/2014 na napenda kumshukuru Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto pamoja na watendaji wake wote kwa mashirikano yao makubwa wanayotupatia.

Mhe. Spika, baada ya kuyasema hayo kwa niaba ya Kamati yangu naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kama kuna maswali yoyote juu ya taarifa hii.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii kuuliza maswali machache kutokana na ripoti hii ambayo tumewasilishiwa na Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto. Kwanza nimpongeze Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri lakini pia niipongeze Kamati kwa ushauri, muongozo na maelekezo ambayo wametoa kwa Wizara, ili kuona kwamba watoto wetu wanapata haki kama wanavyotakiwa kuipata.

Mhe. Spika, kwa kuanzia naomba nianze na Mahkama ya Watoto ambayo Mhe. Waziri ameizungumzia kidogo najua haigusani na Wizara yake moja kwa moja lakini najua serikali inafanya kazi kwa pamoja, hivyo majibu yatapatikana. Kwanza kuna ile *system* ya kusikilizia kesi za watoto ambapo mtoto anatenganishwa mbali na yule mtu ambaye amefanya uhalifu. Sasa wakati tunafanya ziara za kazi wakati niko katika Kamati ya Katiba na Sheria chini ya Mwenyekiti wangu Mhe. Ali Abdalla Ali wakati ule, tulifika katika Mahkama ile na kulikuwa kuna tatizo la kipaza sauti ambacho kinatakiwa kuwa katika ile *system* ambacho kinamfanya yule muhalifu anayeulizwa anatenganishwa na yule mtoto, kipaza sauti kile kinasababisha kwamba wanasikilizana chumba hiki na kile chengine.

Sasa nilikuwa nataka kujua kwamba ni muda mrefu kile kilikuwa hakijapatikana, na tukaiomba serikali kama mfadhili bado hajawa tayari kufadhili kifaa kile tuliomba serikali wanunue kifaa kile ili kuona kwamba kesi za watoto zinasikilizwa kama inavyotakiwa kusikilizwa. Nilikuwa ninaomba kumuuliza Mhe. Waziri, je, *system* ile imeshaanza kufanya kazi, kwani ni muda mrefu sasa tangu imewekwa pale ili ifanye kazi.

Jengine nilikuwa nataka kuzungumzia kuhusu ushughulikiaji wa malalamiko, ukurasa wa 12 ambapo…

Mhe. Spika: Katika sura ya maswali Mhe. Mjumbe.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, swali katika ushughulikiaji wa malalamiko ni kwamba Mhe. Waziri ameeleza kwamba katika mambo ambayo watayapa kipaumbele moja ni kuona kwamba sheria zile ambazo zinakwamisha watoto kupata haki zao zinafanyiwa kazi. Nilitaka kujua ni jinsi gani Wizara imejipanga kulichukulia hatua mara moja ili kuona kwamba hili suala haliwi kikwazo tena kwa watoto, na kama tunavyoona kwamba *ZAFELA* wenyewe wamekuwa wakilipigia kelele sana kuhusu sheria na Kanuni ambazo zinawabana watoto kupata haki zao.

La tatu, Mhe. Spika, nilikuwa naangalia takwimu kidogo nimeona kuna matatizo ya takwimu, na kwa sababu tunatakiwa kuuliza maswali kwa ufupi sitaweza kusema yote, lakini nilikuwa ninamuomba tu Mhe. Waziri ayafanyie kazi takwimu hizi kwa sababu kuna maeneo yanaonesha kwamba hakuna matatizo lakini *in access* kuna matatizo, sisi ambao tunakwenda tunayakuta lakini takwimu hazisemi hivyo. Kwa hivyo, nilikuwa ninamuomba Mhe. Waziri, alifanyie kazi na anambie kwamba atalichukuliaje hatua.

Mhe. Spika, ninakushukuru.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipatia fursa hii, nichukue nafasi hii nimpongeze Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri wa hotuba hii nimpongeze Mhe. Mohammed Mbwana kwa kuwasilisha vizuri maoni ya Kamati yake.

Mhe. Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri kabla ya kufikia siku ya mtoto wa Afrika tarehe 16/06/2014 walianza na *activity* gani ili kuipa nguvu siku hii ya Mtoto wa Afrika. Katika kiambatanisho namba 9 kimeeleza takwimu kwenye kitabu kuhusu uundwaji wa mabaraza ya shehia. Wilaya ya Wete imetupa takwimu ya shehia 32, Wilaya ya Micheweni shehia 27. Ninamuomba Mhe. Waziri aje anambie ni shehia gani na gani katika Wilaya ya Wete, kwa sababu hili tatizo la watoto zipo katika shehia zote.

Mhe. Spika, katika kituo cha kulelea watoto yatima. Kituo hiki kipo hapa Unguja tu, kwa hivyo naomba Mhe. Waziri aje anambie ana mpango gani ambao wameupanga katika kuviendeleza vituo hivi katika Kisiwa cha Pemba, ili na watoto walioko kule Pemba wapate kituo cha kulelewa na waweze kutatuliwa matatizo yao.

Mhe. Spika, Wilaya ya Micheweni inaongoza kwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu. Nimuombe Mhe. Waziri awape kipaumbele watoto hawa wa Wilaya ya Micheweni.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Nashukuru sana Mhe. Spika, mimi naomba niulize maswali mawili matatu na hasa kutokana na kifungu cha 14 kuhusiana na suala la ajira kwa watoto. Kwa kuwa Mheshimiwa Wizara hii inaelewa kuwa tatizo hili limekuwa ni sugu sana, na mpaka hivi leo watoto bado wanaendelea kuwaajiri. Mheshimiwa sheria imepitishwa, lakini je, Wizara yako mpaka sasa hivi imewatia hatiani wazee wangapi ambao wanaowatumia watoto katika biashara wakati umri ni mdogo.

Vile vile Mheshimiwa nikiingia katika ukurasa wa 18 watoto walemavu. Sheria nimeiona ambayo imepitishwa katika Baraza lako Tukufu; sheria namba 9, lakini hivi sasa kwa kweli bado Wizara yako haijafikia malengo ya kuweza kuwahudumia watoto walemavu. Je, Mhe. Waziri ikiwa kama ni hivyo una mkakati gani wa kuweza hasa kwa kutumia sheria hii iliyotungwa hapa kwenye Baraza la Wawakilishi kwa kuweza kuwahudumia watoto wadogo wenye ulemavu.

Mheshimiwa nikienda katika suala la mazingira ya watoto wanaoishi katika hali ngumu. Mheshimiwa hili suala tumelipigia kelele sana na sauti zimetukauka. Mheshimiwa Wizara yako ina mkakati gani hasa katika hiki kipindi

cha bajeti cha juzi tumeanza kukupitishia wewe kuhakikisha kuwa sasa hivi watoto wanaoishi katika mazingira magumu hali hiyo inaondoka mara moja kabla kufika 2015.

Jengine kutokana na hali halisi ilivyo Wizara yako kupata msaada wa Ustawi wa Jamii kwa Watoto. Ningeomba kama ungekuwa angalau na vielelezo viwili vitatu, na kutokana na msaada ambao walioweza kupewa kati ya kinamama na watoto ni misaada mingapi na misaada hiyo ya aina ngapi. Kwa sababu kelele bado ziko nyingi kutokana na kinamama na watoto ambao wanaozaa.

Kwa hivyo naomba sana kuwa nione jinsi gani pamoja na upungufu ambao uliondoshea kuzaa kule ni bure, lakini bado hali imekuwa ngumu, je Mhe. Waziri angalau unapitia sehemu ya wodi ya kinamama kule na ukaona kuna tatizo ukaweza ukawasidia.

Mhe. Spika, ninashukuru nangojea jibu, naunga mkono. Ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, ninashukuru na mimi kunipa fursa hii kuchangia hotuba hii ya Utekelezaji wa Haki na Usawi wa Watoto aliyoiwasilisha hivi punde Mhe. Waziri. Kwanza nimpongeze na yeye kwa uwasilishaji wake mzuri, lakini pia nichukue fursa hii kumpongeza Mwenyekiti ambaye na yeye amewasilisha ripoti ya Kamati vizuri. Mhe. Mwenyekiti, mimi niishukuru serikali na niipongeze kabla kuuliza swali langu, niipongeze serikali kwa kutoa msaada kwa wale wazazi ambao wanajifungua watoto mapacha kuweza kuwasaidia. Hii natoa shukurani.

Swali langu nilitaka kujua Wizara ina mkakati gani au ina mpango gani wa kuwachukulia hatua wale mababa wanaowatelekeza watoto na wakiwaacha wanayumba bila ya kupata mahitaji maalum.

La pili, watoto wenye ulemavu, hawa huwa wanahitaji mahitaji maalum vikiwemo vifaa vya kusomea. Wizara imejipanga vipi kuhusu kuwapatia vifaa hivyo ili watoto hawa na wao waweze kupata elimu ikiwa ni miongoni mwa haki zao za msingi.

La mwisho, ni lile la udhalilishaji wa watoto kijinsia. Mhe. Spika, mimi ninamuuliza Mhe. Waziri hili ni kero kubwa sana ambalo limewakumba watoto wetu. Wizara ina mpango gani, na kwa kuwa suala hili tumeshalisema muda mrefu ya kuweza kupata kile kifaa cha *DNA* ili watoto hawa na wao hizi kesi zao zikaweza kupiga hatua kwa kuwatambua wale ambao wanawafanyia vitendo hivi vya udhalilishaji.

Mhe. Spika, nilitaka kujua hayo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, mimi kwa haraka haraka bila ya kupoteza muda nije na Wizara ya Afya imeongeza vituo vya afya hadi kufikia 164 ambavyo vinatoa huduma kwa watoto na akinamama. Swali langu lipo hapa, hivi vituo vinaweza kuwepo lakini vitendea kazi kama dawa zipo? Na hili suala tumelishuhudia kwa muda mrefu likiwa likitusumbua katika ufuatiliaji.

Swali la pili, niipongeze Kamati sana kwa jitihada iliyochukua kuhusu watoto pacha; shilingi elfu ishirini (20,000) kwa kweli hiki kitendo elfu ishirini napendekezwa ziongezwe, pesa ni kidogo na niiombe Wizara au Serikali kusikiliza kilio cha Kamati, wamefanya kazi ngumu na kazi ya kupongezwa.

Kuhusu suala la Nyumba ya Kulelea Watoto Mazizini; hili suala nyumba inataka iangaliwe kwa hali na mali. Kwa kweli ukiangalia Mwakilishi au Mbunge au Waziri anahitaji kiwanja kukaa Mazizini, hii nyumba iko katika mazingira mazuri lakini inataka kuboreshwa, kutunzwa na kuangaliwa. Na bajeti yake hairidhishi kiasi fulani, mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati hiyo niiombe sana Serikali na Wizara hii nyumba iangaliwe kwa jicho la huruma.

Ni hayo tu Mhe. Spika.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuchangia kidogo. Mhe. Spika, mimi ningeliomba tu, pamoja na maelezo na mambo mazuri ambayo yameainishwa humu. Ningeliomba Viongozi Wakuu wa serikali pamoja na majukumu mengi na mazito ambayo wanayo, wapate wasaa wakatembelee yale maeneo ambayo wapo wale watoto, hususan watoto yatima; ambapo wapo kule wanaendelea na mambo yao ya

kutunzwa. Ningeliomba waende wakawatembelee ili waweze kusikia vilio vyao na waweze kupata fursa ya kusikilizwa moja kwa moja kwa yale mambo ambayo wanayo.

Mhe. Spika, baada ya hapo nilikuwa naomba tu haya ambayo yalikuwa yamezungumzwa humu na haya ambayo yamo humu na mengi ambayo yamesemwa, serikali naomba ichukue hatua za makusudi katika kuhakikisha kwamba haya yanafanikishwa kwa maslahi ya Taifa letu la baadae. Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, mimi sina la ziada nakubaliana na naunga mkono yote ambayo yamewasilishwa. Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii nina masuala mawili au matatu.

Katika ukurasa wa 14 Mhe. Spika, hapa nataka Mhe. Waziri amesema kwamba kuna kupambana na hawa watoto kuhusu ajira, lakini nataka nimuulize pamoja na kupambana na watoto na ajira, je, kuna hatua gani za kuchukuliwa za kisheria kwa wazazi wanaowaachia watoto kufanya kazi na ni watoto wadogo wana haki ya kwenda skuli.

Jengine ukurasa wa 9 unasema kwamba watoto wanaokinzana na Sheria. Hapa Mhe. Waziri alisema watoto wanaokinzana na sheria ni wale wanaotiwa hatiani baada ya kukiuka sheria kwa namna moja au nyengine, lakini watoto hawa akawataja lakini hakutaja ni watoto wa umri gani, kwa sababu alisema kwamba hapa ni watoto wanaokinzana na sheria, lakini kuna chini ya miaka 9 au 10 watoto hawa bado wanaingia hatiani. Kwa hiyo, hapa namuomba Mhe. Waziri watoto hawa wanaoingia hatiani miaka 9 au 10 hawa na wao wanaachiwa bila ya kwenda skuli, huoni hili ni tatizo na wanakosa haki zao.

Jengine Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 35 Shehia ya Ng'ombeni, Shehia ya Mbuguani, Shehia ya Changaweni na Shehia ya Uweleni hapa kidogo ukurasa umenitoka lakini alisema kwamba watoto wale, Mhe. Spika, kidogo imenitoka lakini katika shehia alizozitembelea watoto waliokuwa…

Mheshimwia kidogo imenitoka kwa sababu unaniambia tufanye haraka kwa sababu…

Mhe. Spika: Mambo ya haraka haraka yana matatizo kidogo.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Mhe. Spika, naona bora niachie kwa sababu sioni ule ukurasa nikiupata Mheshimiwa nitanyanyuka. Ahsante.

Mhe. Spika: Nakuomba radhi Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi kwa kuomba tufanye haraka haraka, kwa hiyo sasa nimuombe Mhe. Marina Joel Thomas naye aulize maswali.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii kwanza nampongeza Mhe. Waziri kwa ripoti yake nzuri yenye *data* za kuridhisha pamoja na watendaji wake.

Mimi nitauliza katika kiambatanisho Nam. 6 ambacho kimeeleza vituo hivi vya kulelea watoto.

Mhe. Spika, kuna vituo vya aina mbili; kuna jumuiya na watu binafsi. Je, Mhe. Waziri katika jumuiya hizi ambazo naamini jumuiya hizi zinatafuta misaada katika taasisi mbali mbali nje na ndani ya nchi, anazisimamia vipi ili kuona kwamba ile misaada ambayo wanayoipata kutoka taasisi mbali mbali inawafikia walengwa. Na hizi taasisi binafsi ambazo wamejitolea kuwahudumia hawa watoto, je, anazisaidia vipi kuona kwamba zinaendelea na kukua vizuri.

Jengine Mhe. Spika, humu kwenye kitabu kumeelezwa changamoto nyingi tu kwa kila kipengele kama watoto wenye ulemavu, huduma za msaada wa kisheria kila kipengele kuna changamoto mbali mbali ambazo zimeelezwa. Nimuulize Mhe. Waziri je, amejipanga vipi kuzitatua changamoto hizi? Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, mimi nitauliza haraka haraka sana katika ukurasa wa 34 kuna kiambatanisho kule Nam. 4(a) ambacho kinaeleza kuhusu watoto wanaoishi katika mazingira magumu zaidi waliotambuliwa katika Wilaya tano za Unguja na Wilaya tatu za Pemba.

Mhe. Spika, Shehia zote zilizofanywa utafiti huu ni 50 kwa Unguja na Pemba, na jumla ya watoto waliokutikana katika mazingira hayo magumu zaidi ni 9305, kati ya hao 5690 ni wanaume na 3615 ni wanawake. Sijui Mhe.

Waziri baada ya kuona utafiti huu ameandaa sera gani za kuona kwamba watoto hawa wenye mazingira magumu zaidi wanashughulikiwa ipasavyo ili wapate haki zao kikamilifu.

Suala la pili katika hayo mazingira magumu, naamini hata ikiwa kuna mazingira magumu ya mtoto pia yanatokana na mazingira magumu ya nyumba ya wazee. Na utaratibu wetu hivi sasa ulioko ni kuwa mtoto anapopelekwa skuli huwa ni lazima achangie, na wazazi hawana pesa na ni wengi tu. Kwa hivyo, watoto mara nyingi huwa wanakosa haki yao ya lazima. Kwa hivyo, Mhe. Waziri haoni kuwa iko haja ya kurejesha ile hali ya makusudi ya kufanya Mapinduzi hapa Zanzibar ya wanafunzi kupatiwa elimu bila ya malipo mia juu ya mia, waondolewe na mambo haya ya uchangiaji ambayo yanawakosesha haki zao.

La tatu kumjenga mtoto katika silka, mila, desturi ya kijamii ni jambo muhimu sana, kwa sababu Mhe. Waziri alisema kuwa *UVIKIUTA* ni Umoja wa Kikristo Tanzania, na watoto wetu wanashiriki katika umoja huu wa vijana, hatuoni kuwa hakuna ulazima wa watoto ambao wana dini nyengine kuliko hii taasisi inavyoelekeza kujiunga katika taasisi kutokana na kuwa huko wanakokwenda watabadilikiwa kimazingira ya kidini.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kutoa maelezo ya hapa na pale kulingana na maswali waliyoniuliza Waheshimiwa Wajumbe.

Kwanza nikianza na Mhe. Makamu Mwenyekiti namshukuru sana kwa mchango wake. Makamu Mwenyekiti ametusaidia sana kutupa maelekezo mbali mbali, ushauri, mwongozo na kadhalika.

La kwanza ninalotaka kumjibu alisema Makamu Mwenyekiti kwamba mwaka jana hatukuleta taarifa hii ya utekelezaji wa haki za mtoto. Ni kweli Mhe. Spika, nakubaliana naye, kwa sababu tuliileta hapa taarifa na wewe unakumbuka kwa bahati ikawa ina makosa mengi na ikabidi taarifa ile tuirejeshe, sasa ninachotaka kumuahidi kwamba nitajitahidi taarifa ya mwaka 2013 ipatikane na nitaileta katika kipindi kinachokuja tukijaaliwa ili Waheshimiwa waione, waisome na waweze kutusaidia. Hilo ni moja.

Mhe. Spika, kuna mambo mengi lakini pia amezungumzia kuhusu mkakati wa udhalilishaji. Hoja binafsi ililetwa hapa na Mhe. Mgeni Hassan Juma nakumbuka na sisi tunaifanyia kazi ile hoja, tunaandaa Kanuni za kutekeleza ile sheria Nam. 6 ya mwaka 2011, lakini bado tunatoa vipindi mbali mbali kuwaelimisha wenzetu, wazee tunawaelimisha juu ya udhalilishaji wa watoto, vipindi vya redio na vipindi vya televisheni. Tukipata nafasi ya kufanya mikutano lakini kubwa ni kwamba kesi ikifika Mahakamani mwisho wake tunakwama. Mtu anaweza akahukumiwa miaka pengine 25 akakaa mwaka mmoja haujamaliza vyema ule mwaka akatolewa nje, na akishatolewa anatamba kuonesha kwamba yeye ni hodari wa mambo yake.

Sasa nadhani jambo kubwa sisi Waheshimiwa Wajumbe, wazee tulioko huko na wazee wengine nao wanawabaka watoto wao ndani ya majumba yao, kwa kweli ni mambo ya kusikitisha sana, lakini jambo hili sisi tunalifanyia kazi kwa moyo mmoja ili kuhakikisha kwamba huu udhalilishaji unaondoka kabisa.

Mhe. Spika, wizara inachukua jitihada mbali mbali; tunafanya semina, tunafanya mafunzo, tunafanya makongamano kuhusu suala la udhalilishaji na kama watu wanakaa wanaangalia vipindi vyetu basi wataona zile jitihada zetu. Pia nimuombe Mhe. Makamu Mwenyekiti kwamba ni kweli bajeti yetu ni ndogo tunayoipata sisi, lakini pamoja na hayo tutafanyaje sasa, kwani tunatoa misaada midogo midogo kwa kadri ya bajeti yetu. Kwa hivyo, naomba tuvumiliane hivyo hivyo kidogo ilimradi tuone kwamba kazi zetu zinakwenda siku hadi siku.

Mwisho nataka nimwambie Makamu Mwenyekiti kwamba miongozo aliyotupa, ushauri aliotupa, *inshaallah* tutaufanyia kazi ili tuone tunakwenda vipi hatua baada ya hatua.

Nikitoka hapo nataka sasa niende kwa Mhe. Wanu Hafidh Ameir ametuuliza Mahakama ya Watoto je imeshapata kipaza sauti?

Mhe. Spika, mimi nataka nikwambie wazi wazi kwamba bado kipaza sauti hakijapatikana, lakini jitihada zinafanyika ili kipaza sauti kipatikane. Ushauri kuwaelekeza watoto tunawaelekeza kwamba wakifika pale wasiogope, wasiwe na wasi wasi ili waweze kutoa ushahidi wao bila ya wasi wasi wowote, lakini bado kipaza sauti hakijapatikana.

Kuhusu ushughulikiaji wa malalamiko ya watoto kwa kweli tunashughulikia, kuna malalamiko mengi ya watoto, wengine wanapokwisha kuwaacha kinamama hawawashughulikii tena watoto, hawawapatii chakula, hawawapatii nguo, hawashughuliki kwa afya zao wala chochote kile inakuwa kama ni kumkomoa yule mama. Yeye mwenyewe ndiye aliyeacha halafu yeye mwenyewe analeta matatizo kama hayo, lakini pamoja na hayo tunawaita kinababa wale tunawafahamisha, tunawaelekeza kwamba jamani haifai, tuwashughulikie watoto wetu, ni watoto wetu wenyewe kwa nini tuwadharau tuwaache wapate shida. Kwa hivyo, ushughulikiaji wa malalamiko kwa ujumla tunayashughulikia.

Vile vile, anasema takwimu tuzifanyie kazi, *Inshallah* takwimu tutazifanyia kazi ili ziende vizuri.

Mhe. Spika, nikiendelea nakuja kwa Mhe. Viwe Khamis Hamad, yeye ameniuliza swali hapa kabla ya kufikia Siku ya Mtoto wa Afrika tulifanya nini?

Kwanza kama kawaida tuliendelea na kutunga Mabaraza yetu ya Watoto halafu kwa bahati nzuri tulifanya mafunzo maalum kwa watoto ili wajue haki zao na sio kujua haki zao tu wajibu wao watoto pamoja na namna ya kujikinga na udhalilishaji kwa Wajumbe wa Baraza la Watoto, na kazi hiyo tuliifanya Kitogani Wilaya ya Kusini. Baadae tarehe 15 tulisoma *statement* ya Maadhimisho ya Siku ya Watoto kwenye vyombo vya habari. Ile siku ya kilele yenyewe hasa tulifanya sherehe viwanja vya Ziwani na tukawajumuisha wanafunzi wa skuli za maandalizi, wanafunzi wa skuli za msingi na kati na Katibu Mkuu wetu wa Uwezeshaji ndiye aliyekuwa mgeni rasmi. Na ujumbe wa mwaka ulikuwa "*elimu bora isiyokuwa na vikwazo ni haki ya kila mtoto*". Hayo tuliyaeleza uwanjani, kwa hivyo hizo ni shughuli tulizofanya Mhe. Viwe kabla ya kufikia ile Siku ya Mtoto.

Mhe. Viwe Khamis Hamad, anasema kwamba kituo cha watoto yatima Pemba bado hatujapata, ni kweli sisi hatujapata Pemba kituo cha kulelea watoto yatima, lakini jambo hili tumeshalizungumza kwenye wizara, na tukijaaliwa wakati wowote tukija tukipata pesa za kujengea tutaweza kuwachukua watoto yatima. Sasa hivi utaratibu uliopo watoto yatima huwa wanatolewa kutoka Pemba wanaleta katika kituo cha Mazizini Unguja. Tunao pale watoto yatima ambao wanatoka Pemba, lakini nia yetu hasa ni kujenga kituo cha kulelea watoto yatima huko Pemba tukipata fursa wakati wowote *inshaallah* tutajenga.

Vile vile, Mhe. Viwe, anasema Wilaya ya Micheweni tuipe kipaumbele, ni juzi tu hapa tulivyokuwa na bajeti Mhe. Subeit Khamis Faki alisema kwamba tutakuwa na mpango gani sisi wa kudumu wa kuwasaidia wananchi wa Micheweni. Mpango wa kudumu kwa sasa hivi kwa kweli mpango tulionao ni wa kuwawezesha watu kimikopo, tutawakopesha wazazi wa watoto hawa wa Micheweni ili waweze kufanya miradi mbali mbali waweze kuwasaidia watoto wao, lakini Mhe. Viwe nakuomba pia tushirikiane katika suala hili, kwa sababu hali ngumu sio Micheweni tu, lakini tena kuna ile hali ngumu zaidi, lakini hali ngumu imeenea, sasa tukifanya hivyo tukawashajihisha watu wakaunda vikundi vya ushirika, wakafanya kazi wakajituma basi tutawapa mikopo na mambo yao yatakuwa mazuri.

Nikumuacha Mhe. Viwe, nataka sasa niende kwa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk. Mhe. Makame Mshimba anasema watoto wenye ulemavu tunawasaidia nini?

Watoto wenye ulemavu tunasaidia kwanza kuwaambia wazazi wao kwamba watoto wenye ulemavu wasiwaweke ndani wakawaficha, wanapokwenda watu wawatoe wa kustahiki kupewa msaada apate msaada, wa kustahiki kupewa kigari apate kigari, wa kustahiki kusoma asome na kwa bahati nzuri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali tunashirikiana vizuri watoto wenye ulemavu sasa hivi wanashughulika, wanasoma na wao.

Kuna mambo ya nundu za mikono sijui za nini, lakini watoto wanasoma. Mimi mwenyewe niliwahi kwenda kwenye shughuli mtoto mwenye ulemavu anasoma taarifa yake mimi mwenyewe nilipukutikwa na machozi anasoma vipi wakati haoni, lakini kuna alama maalum zile wanazotumia, kwa hivyo, watoto tunawashughulikia.

Watoto wenye mazingira magumu. Siwezi kusema hapa kwamba misaada mingapi tuliyoitoa Mhe Makame Mshimba Mbarouk, lakini tunawasaidia. Watoto wenye mazingira magumu kila tunapopata msaada tunasimama sisi wenyewe kwenye wizara kuhakikisha kwamba ule msaada unawafikia wale watoto wenye mazingira magumu na sisi wenyewe wakati mwengine huwa tunakwenda tunapeleka misaada kwa watoto hao. Kwa mfano mabuku ya kusomea, *uniform* za kuvaa, mifuko ya kutilia mabuku yao na kadhalika. Sasa mambo kama haya hata Waheshimiwa Wawakilishi, wenyewe katika majimbo yao wanaweza wakasaidia kumpa mtoto buku la kuandikia si

pesa nyingi sana, kumpa kalamu si pesa nyingi. Kwa hivyo, sisi watoto hao wenye mazingira magumu sisi wizara, lakini na sisi Wawakilishi hapa tujitahidi kuwasaidia wenzetu hao.

Vile vile, nimeulizwa kama nishapita Hospitali angalau siku moja nikaona na kuwafariji watu na kadhalika. Nishapita wala si mara moja, mara nyingi tu napita Hospitali, kuna siku yetu maalum huwa tunakwenda tunawakagua wagonjwa na tunawapatia zawadi, wakati mwengine tuna soda tunawapa na kuwapa pole ndio jambo kubwa.

Mhe. Panya Ali Abdalla, kwanza ametupa pongezi, mimi nashukuru sana, misaada kwa wanaozaa mapacha kweli shilingi 20 elfu hazitoshi, lakini tutafanyaje, afadhali tuwe na kitu kidogo tuwawezeshe wenzetu hicho hicho kidogo tulichonacho.

Watoto wenye ulemavu kupatiwa vifaa. Watoto wenye ulemavu huwa wanapatiwa vifaa, ingawaje havitoki katika ofisi yetu, lakini Wizara ya Afya huwa tunashirikiana kwa pamoja watoto wenye ulemavu wanapewa vigari, wanatembelea vigari, wanapewa na mambo mengine yanayostahiki na hili suala la *DNA* Waheshimiwa, bado *DNA* haijapatikana na kwa kweli mashine hii ni ghali sana. Sasa tunakosa ushahidi, lakini mtu anakuwa anaonekana, tayari keshakutwa na mtoto wa watu shuka mkononi, karoa anakimbia, anaambiwa huyo anatoka kumbaka mtoto, halafu tunasema hakuna ushahidi tunasubiri *DNA.* Jamani kwa kweli tunawaumiza watoto wetu, tunaumiza Taifa letu kwa ujumla.

Kwa hivyo, tujitahidi wazazi tuwe karibu sana na watoto wetu, mtoto ukiona humuoni masaa yamepita, basi lazima utafute mtoto yuko wapi, sio unamwambia mtoto nenda kacheze tu, dunia hii sasa hivi sio ya hivyo.

Sasa nije kwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub, anasema hivi vituo vya mkono kwa mkono dawa zipo au tunaweka tu vituo hivi. Mhe. Jaku Hashim, vituo vya mkono kwa mkono zipo dawa na watoto wengine hulazwa pale na wanahudumiwa bila ya kutozwa pesa. Tumewahi kuona sisi hapa hapa Hospitali ya Mnazi Mmoja mtoto kaletwa kaharibiwa vibara sana, ikabidi mtoto achukuliwe alazwe pale Hospitali. Lakini pamoja na hayo, tukaambiwa hakuna ushahidi kesi ilipofika Mahakamani, mtoto kaumizwa, yaani ushahidi wa wazi halafu unasema hakuna ushahidi, ushahidi gani, kwa sababu huwezi kumkuta mtu hivi hivi anafanya tendo lile kwa sababu wanajificha ili wasionekane.

Serikali inachukua hatua mbali mbali kama hivyo vituo vya mkono kwa mkono sasa hivi vimeenea Unguja na Pemba, madawa yapo yananunuliwa na kadhalika na wahisani wanatusaidia.

Mhe. Spika: Mheshimiwa tujitahidi muda umekwenda kidogo.

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto: Sawa Mheshimiwa. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, anasema twende tukawasikilize watoto wenye matatizo maalum. Tutakwenda kuwasikiliza, ili tujue wana matatizo gani kama kuweza kuwasaidia tutawasaidia, kama tunaweza kuwapa ushauri tutawapa ushauri, kama kuna maelekezo tutawapa maelekezo alimradi tutakwenda na sisi kuwaona.

Mhe. Salim Abdalla Hamad, anasema hao watoto wenye mazingira magumu zaidi tuwafanyeje? Watoto hao wenye mazingira magumu nao tunawapa misaada kwa kadiri tunavyoipata. Tunawapa misaada pale tunapopata misaada wala hatuisukumi tu kuwa msaada ushapatikana tukasema basi wapelekee, tunakwenda sisi wenyewe kuwapa misaada hiyo.

Vile vile, anasema kwamba zamani ilikuwa elimu bila ya malipo. Je, sasa hivi kwa nini kila kitu unaambiwa ununue? Mpaka sasa hivi elimu ni bila ya malipo isipokuwa wazazi wanachangia tu, kuchangia kwa mfano unanunua kitabu cha mwanao, mkoba wa mwanao na mambo mengine, lakini kwa ufupi elimu ni bure, mishahara walimu wanalipwa na Serikali, kuchangia tu imo.

Mhe. Spika, hata Wizara ya Afya pia tunachangia sio kama daktari tunamlipa hasa, lakini tunachangia na kadhalika.

Sasa kama mtoto huyu hana malipo hatakiwi afukuzwe skuli. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali yenyewe inasema kwamba mtoto kama kakosa ada usimfukuze ndio hana kwa wakati ule na hawa wazee lazima tuwaangalie, wazee wengine wana uwezo, lakini wengine hawana uwezo, kwa hivyo, tusiwafukuze watoto tuwaachie wasome.

Kweli kipindi cha nyuma kulikuwa na tabia hiyo, lakini sasa hivi jambo hilo limepungua sana na hao watoto wenye mazingira magumu zaidi ndio na wao kabisa wanakwenda hawalipishwi hasa, wanakwenda wanasoma hata kama wana matatizo gani ya kulipia hawalipishwi chochote.

Mhe. Spika, mimi nataka niseme kwamba, suala hili la watoto ni pana sana, malezi yana matatizo,yaani makuzi ya mtoto yana matatizo kuanzia unapomzaa ile siku ya mwanzo mpaka kufikia miaka 18 bado ni mtoto, ana mahitaji maalum; anatakiwa asome, apate afya bora, chakula bora na malazi bora, kwa hivyo, lazima tujitahidi sisi kuzungumza na wazazi tulionao katika majimbo yetu na sisi tunapopata nafasi huwa tunazungumza nao kuwaambia jamani mtoto ndio hazina kuna msemo wa Kiswahili unaosema:

"Masikini na mtoto, tajiri na mali yake".

Mhe. Spika, naomba ikiwa wengine sikuwajibu vizuri wanisamehe, naomba kuwasilisha.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri, Taarifa imewasilishwa, majibu yametolewa, Waheshimiwa Wajumbe, sasa taarifa hiyo ipokelewe rasmi. Waliopokea taarifa wanyanyule mikono. Wanaokataa taarifa, waliopokea wameshinda.

(Taarifa ilitolewa ipokelewe)

(Taarifa ilipokelewa na kukubaliwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nikushukuruni kazi kubwa mmeifanya tangu tarehe 14 mwezi uliopita wa Mei, hadi leo hii. Katibu anatueleza kwamba shughuli zote za mkutano huu sasa zimemalizika. Basi nichukue nafasi hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe na sasa nimuombe Mhe. Makamu wa Pili wa Rais. Karibu sana. *(Makofi)*

KUAKHIRISHA BARAZA

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutujaalia neema ya uhai na uzima na kutuwezesha kukutana tea katika Mkutano huu wa 16 wa Baraza la Wawakilishi. Pia, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuijaalia nchi yetu kuendelea kuwa na amani, utulivu na salama ambayo ni hazina yetu kubwa inayohitaji kuenziwa na kila mmoja wetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu atuzidishie umoja na mshikamano ili tuweze kuitunza amani hii na kudumisha utulivu tulionao nchini mwetu daima milele.

Mhe. Spika, kwa dhati kabisa napenda kukushukuru na kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika, Wenyeviti pamoja na Wasaidizi wako wote kwa namna mnavyoendelea kuliongoza Baraza hili tukufu kwa umahiri na umakini mkubwa. Bila shaka uongozi wenu huo umesaidia sana kuyafikia malengo ya mkutano wetu huu wa 16 kwa mafanikio makubwa.

Mhe. Spika, pia, nawashukuru sana Waheshimiwa Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa maelekezo yao yaliyojaa busara kwa wizara na ofisi zetu ambayo yamechangia sana katika kuongeza kasi na umakini wakati wa kupanga na kutekeleza majukumu yetu. Aidha, shukurani nyingi sana ziwaendee Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu kwa michango yao yenye upeo mkubwa katika kuijenga nchi yetu na kuiletea maendeleo katika nyanja zote.

Mhe. Spika, kwa nafasi ya pekee nachukua fursa hii kumpongeza Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake uliojaa hekima na busara ambao umekuwa ni chachu ya uwajibikaji kwetu katika kufikia hatua kubwa za kimaendeleo zinazoonekana hivi sasa katika nchi yetu. Vile vile, nampogeza sana Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar kwa kuendelea kumshauri vyema Mhe. Rais katika kuiongoza nchi yetu hii. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu awazidishie nguvu na uwezo wa kuendelea kuitumikia nchi hii kwa hekima na busara zaidi.

Mhe. Spika, natoa shukurani maalum kwa Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu na Watendaji wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa bidii kubwa wanayoionesha katika

kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Kwa hakika wananchi wamejenga imani na matumaini makubwa kwa viongozi wao hawa kutokana na hatua kubwa za kimaendeleo tunazoendelea kuzipata.

KUDUMISHA AMANI, UTULIVU NA MSHIKAMANO

Mhe. Spika, ili nchi yoyote iweze kufanikiwa kupata maendeleo endelevu, ni lazima kuwepo na amani na utulivu. Hivyo, suala la kudumisha amani, utulivu na mshikamano hapa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla lina umuhimu mkubwa sana katika ustawi wa nchi na wananchi wetu. Tumeshuhudia mifano mingi duniani kwa nchi ambazo zimekosa amani na utulivu namna nchi hizo zilivyovurugika kwa maelfu ya watu kupoteza maisha yao, maelfu kuwa wakimbizi, kuwepo kwa udhalilishaji mkubwa wa kijinsia hasa kwa wanawake na watoto na uharibifu wa miundombinu ya nchi na mali za wananchi.

Mhe. Spika, ukichunguza kwa makini utagundua kwamba, uvunjifu huo wa amani unasababishwa na watu wachache kwa maslahi yao binafsi ya kujilimbikizia mali, uroho wa madaraka na kupalilia tofauti za kidini, ukabila na umajimbo.

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio makubwa tuliyopata katika kuenzi umoja na amani, hivi sasa ndani ya nchi yetu zimejitokeza kila dalili kwa baadhi ya watu wachache kufanya vitendo vinavyoashiria uchochezi na uvunjifu wa amani jambo ambalo halikubaliki hata kidogo. Ni vyema kwa wenzetu hawa wakaelewa kwamba ni rahisi sana kuvunja amani, lakini ni gharama kubwa sana kuirudisha amani pindi ikitoweka. Hivyo, natoa indhari kuwa, wote tunapaswa kuwa makini na kauli na vitendo vyetu hasa sisi viongozi wa kisiasa, kijamii na kidini ili kauli na vitendo hivyo visiwe chanzo cha uvunjifu wa amani na utulivu hapa nchini.

Mhe. Spika, napenda kuwakumbusha viongozi wenzangu kwamba sisi ni wachunga na tutaulizwa juu ya tunavyovichunga. Hivyo basi, tusijisahau tunapokuwa na wafuasi wetu katika mazingira tofauti kuwakumbushia jukumu la kuilinda na kuidumisha amani tuliyonayo. Nawaomba sana tusitoe nafasi kwa wale wachache miongoni mwetu wanaochochea mifarakano kwani kufanya hivyo wataivuruga nchi yetu na kudumaza maendeleo yetu. Hatutavitendea haki vizazi vyetu kama tutaiacha nchi hii kuwa katika hali ya vurugu na uvunjifu wa amani.

Mhe. Spika, Serikali inasikitishwa sana na kitendo cha kihalifu kilichotokea hivi karibuni cha mlipuko wa bomu katika eneo la Darajani Mjini Unguja na kusababisha kifo cha mtu mmoja na watu wengine saba (7) kujeruhiwa, wote wakiwa hawana hatia. Serikali inatoa mkono wa pole kwa familia ya mtu aliyepoteza maisha katika mlipuko huo na tunamuomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amin.*

Aidha, tunawaombea wale wote waliojeruhiwa katika tukio hilo wapone kwa haraka ili warudi katika shughuli zao za kawaida.

Mhe. Spika, tukio hili ni la kushtusha na la kusikitisha lililotokea nchini kwetu ambapo bomu la kivita limetumika kufanyia vitendo vya kihalifu. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inalaani kwa nguvu zake zote kitendo hiki cha kihaini na inaendelea kulifanyia uchunguzi tukio hili na kuwasaka wale wote waliohusika ili hatua kali za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi yao. Aidha, Serikali kupitia vyombo vyake vya ulinzi na usalama imejipanga vizuri kudhibiti vitendo kama hivi visitokee tena katika nchi yetu. Natoa wito kwa wananchi kutoa mashirikiano makubwa kwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama kwa kutoa taarifa ili kuwafichua wahalifu hawa wasioitakia mema nchi yetu.

Mhe. Spika, napenda kuwathibitishia wananchi kwamba nchi yetu bado ipo katika hali ya salama, amani na utulivu, hivyo, waendelee kufanya shughuli zao bila hofu. Vile vile, kwa wageni wetu pamoja na watalii waliopanga kuja kutembelea nchi yetu waendelee kuja bila hofu. Nchi yetu bado ni salama.

Mhe. Spika, napenda kuwatanabahisha viongozi wenzangu na wananchi kwa ujumla kwamba hivi sasa tupo katika kipindi cha muendelezo wa mchakato wa kupata Katiba Mpya ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia, kipindi cha matayarisho kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 2015. Hivyo, tunapaswa kuwa makini na kuchukua tahadhari zote kwa kauli na vitendo vyetu kwa wakati wote ili kauli na vitendo vyetu hivyo visiwe chanzo cha kuleta chuki na uhasama miongoni mwetu. Inatupasa tuelewe kwamba mambo yote katika nchi yetu yanaendeshwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni tulizozitunga sisi wenyewe.

Hivyo, hatuna budi kuzifuata Sheria na Kanuni hizo. Tukifanya hivyo, nchi yetu itabaki kuwa na umoja, upendo na mshikamano na hatimaye kupata maendeleo tuliyoyakusudia. Nawasihi sana Wajumbe wa Bunge Maalum la Katiba kuendelea kuwa wamoja na mshikamano ili tukienda kwenye Bunge Maalum mwezi Agosti, twende na sauti moja itakayotuwezesha kupata Katiba Mpya ambayo itakuwa na manufaa na maslahi kwa Zanzibar. Katiba Mpya ndiyo itakayoondoa kero nyingi tunazo zilalamikia kila siku.

MATUKIO MUHIMU:

Mripuko wa Maradhi ya Homa ya Dengue*:*

Mhe. Spika, nchi yetu hasa Jiji la Dar-es-Salaam lilikumbwa na mripuko wa maradhi ya homa ya dengue. Kutokana na mripuko huo Zanzibar nayo imekumbwa na wasiwasi wa kujitokeza watu walioambukizwa maradhi haya. Kwa mujibu wa maelezo ya kitaalamu, maradhi haya yanasambazwa na mbu anayeuma wakati wa asubuhi hadi jioni. Mbu hawa wanazaliana katika maji safi yaliyotuama. Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Afya ni kwamba kwa upande wa Zanzibar watu 11 walionekana kuwa na dalili za ugonjwa huo, lakini baada ya uchunguzi wa kimaabara 9 hawakuthibitika kuwa waliathiriwa na ugonjwa huo, lakini wawili ndio waliothibitika na walitibiwa na sasa hali zao ni nzuri.

Mhe. Spika, napenda kutoa wito kwa wananchi wote kufuata masharti ya afya na kutunza mazingira yetu ili kuhakikisha mbu huyu anakosa maeneo ya kuzalia na anatoweka katika maeneo yetu. Aidha, tuchukue tahadhari na kumuwahisha mgonjwa anayeonesha dalili za ugonjwa huu katika vituo vya afya ili kunusuru maisha yake na kudhibiti kuenea kwa maradhi haya.

Migogoro katika Jamii:

Mhe. Spika, kutokana na kuongezeka kwa shughuli za kiuchumi na kijamii na nchi yetu kuwa na rasilimali ndogo ya ardhi, bado kumejitokeza migogoro inayohusiana na umiliki wa ardhi kwa shughuli za kilimo, biashara na uwekezaji. Serikali itachukua kila juhudi kuhakikisha migogoro hii inamalizika na kuondoka kabisa. Tunahitaji mashirikiano na masheha, madiwani, viongozi wa Serikali pamoja na wanasiasa na wananchi kwa jumla wakati Serikali inaendelea na ukamilishaji wa mpango wake wa matumizi bora ya ardhi utakaosaidia kupunguza migogoro iliyojitokeza. Zimeonekana dalili kuwa baadhi ya migogoro hii kutolezwa na baadhi yetu wanasiasa kwa sababu binafsi za kisiasa. Naamini kwamba kama wote tutashirikiana kwa dhati kwa nia ya kuiondoa migogoro hii tutafanikiwa kwa kiwango kikubwa. Inawezekana kama wote tutatimiza wajibu wetu.

Migogoro baina ya wananchi na wawekezaji:

Mhe. Spika, kumekuwepo na migogoro ya ardhi baina ya wawekezaji na wananchi kwa baadhi ya maeneo. Serikali imejitahidi sana kuwavutia wawekezaji kuja kuwekeza nchini mwetu. Nia ya kufanya hivyo kwanza ni kuongeza mapato ya Serikali, lakini pili, kuongeza ajira kwa vijana wetu. Ni ukweli usiopingika kuwa sekta hii binafsi ndiyo inayotoa ajira nyingi. Hivyo, ningewasihi wananchi waache kuwabeza wawekezaji hawa ambao tumewaita wenyewe ili waje kushirikiana nasi katika kukuza uchumi wetu na kuongeza ajira kwa vijana wetu.

Mhe. Spika, jambo la kusikitisha ni kuwa baadhi ya wawekezaji wetu, hasa wa mahoteli, huajiri watu kutoka nje ya nchi yetu na kuwaacha watu wetu ambao wana taaluma sawa na hao kutoka nje. Ningependa kuwasihi wawekezaji hao kuacha mara moja tabia hiyo kwani hawawatendei haki wenyeji. Naziomba taasisi husika, kama vile Kamisheni ya Kazi, Kamisheni ya Utalii na Uhamiaji kuliangalia suala hili kwa umakini mkubwa. Kazi ambayo inaweza kufanywa na Mzanzibari kusiwe na haja ya kuajiriwa mtu kutoka nje ya nchi.

Matayarisho ya Uchaguzi Mkuu wa 2015:

Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar tayari imeanza rasmi maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa 2015. Kazi hiyo imeanza kwa kufanya uchunguzi wa idadi, majina na mipaka ya majimbo ya uchaguzi Zanzibar kama inavyoelekezwa na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Aidha, tume inaendelea kupokea maoni ya wadau wa uchaguzi juu ya kazi ya uchunguzi wa idadi, majina na mipaka ya majimbo ya uchaguzi kutoka kwa wadau mbali mbali wakiwemo Vyama vya Siasa, Asasi za Kijamii, Vyombo vya Ulinzi na Usalama, Taasisi za Serikali,

wawakilishi, wabunge na madiwani pamoja na wananchi wote katika wilaya husika. Hivyo, tunawaomba wananchi kujitokeza kwa wingi wakati wa utoaji wa maoni hayo tukiwa katika hali ya amani na utulivu.

Mhe. Spika, Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar imeendesha kazi za uandikishaji wa wapiga kura wapya na uendelezaji wa Daftari la Kudumu la wapiga kura. Kazi hiyo ilianza katika mwezi wa Juni, 2013 Mkoa wa Kaskazini Unguja na ilimalizika katika mwezi wa Novemba, 2013, Mkoa wa Kusini Pemba. Zoezi hilo lilifanyika kwa kuwaandikisha wananchi wote waliojitokeza ambao wana sifa za kupiga kura kwa Uchaguzi Mkuu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, aidha, tume ilitoa nafasi kwa wananchi kufanya uhakiki wa Daftari la Wapiga Kura katika vituo vilivyotumika kuandikisha wapiga kura hao ili kuona usahihi wa taarifa zao na uhalali wa wapiga kura hao. Pia, tume ilitoa fursa ya kuweka pingamizi juu ya wale waliopoteza sifa za kuwemo katika daftari, ili daftari liwe na wapiga kura wenye sifa za kupiga kura. Vile vile, Tume ya Uchaguzi itaendesha zoezi jengine la uandikishaji wa wapiga kura kwa wananchi ambao walikosa nafasi ya kujiandikisha katika awamu zilizopita. Lengo ni kuhakikisha kila anayestahiki kupiga kura anapata haki yake hiyo ya kidemokrasia.

Udhalilishaji wa kijinsia:

Mhe. Spika, katika miaka ya hivi karibuni, vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia hasa kwa wanawake na watoto vimeshamiri sana katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Tafiti zinaonesha kwamba watoto wa jinsi zote hawako salama na udhalilishaji huu. Wafanyaji wa vitendo hivi ni watu wa karibu wa watoto hao ambao wanategemewa kuwa ni walezi na walinzi wao. Hebu tujiulize tunatengeneza jamii ya namna gani na watoto wetu tunawaandalia hatma gani? Bila ya shaka, jitihada zaidi za pamoja bado zinahitajika katika kupambana na tatizo hili ili kukiepusha kizazi chetu kuangamia kutokana na janga hili.

Mhe. Spika, Serikali kwa upande wake imekuwa ikichukua jitihada kadhaa katika kupambana na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ikiwa ni pamoja na kufanya tafiti zinazohusiana na matokeo ya udhalilishaji wa kijinsia ili kujua kiwango chake, kuzifanyia kazi sheria, sera pamoja na kutekeleza programu mbali mbali ili kupunguza kasi ya vitendo hivi nchini. Aidha, Serikali imesimamia uanzishaji wa mifumo ya kupambana na vitendo hivi kuanzia ngazi ya shehia hadi Taifa pamoja na kuweka miongozo ya namna ya kuyashughulikia na kutoa huduma kwa waathirika wa vitendo hivyo.

Mhe. Spika, kupitia Baraza lako hili Tukufu, naomba kuendelea kutoa wito kwa jamii kutovifumbia macho vitendo hivi kwa kuvipatia utatuzi na usuluhishi katika ngazi ya familia au jamii bali wavitolee taarifa katika vyombo husika ili wahusika waweze kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria. Aidha, naomba wananchi wasipuuze suala la kwenda Mahakamani kutoa ushahidi kwani ndio njia pekee itakayopelekea wahalifu hawa kutiwa hatiani na hatimae kuvitokomeza vitendo hivi vya kinyama katika jamii yetu. Vile vile, Serikali inawataka kuacha mara moja wale wote wanaojishughulisha na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia kwani Serikali haitamuonea huruma mtu yeyote atakayepatikana na hatia.

VIPAUMBELE VYA SERIKALI:

Mhe. Spika, katika kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi wake, kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015, Serikali itaendelea kuvifanyia kazi vipaumbele ilivyojiwekea katika sekta za kiuchumi na kijamii kama vilivyoainishwa katika Hotuba ya Bajeti ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar 2014/2015, ikiwa ni pamoja na kuimarisha miundombinu ya kiuchumi na kijamii. Kuimarisha huduma za kijamii kama vile elimu, afya bora na upatikanaji wa maji safi na salama. Kuimarisha huduma kwa makundi maalum hasa wazee wasiojiweza, watoto na watu wenye ulemavu. Kuimarisha mazingira ya biashara kwa kuondosha vikwazo visivyo vya lazima na kupunguza urasimu. Kuiendeleza sekta binafsi hasa katika uzalishaji na utoaji wa huduma muhimu kupitia ushirikiano baina ya Serikali na Sekta Binafsi *(PPP)*. Kuharakisha upatikanaji wa ajira bora hasa kwa vijana na kuimarisha utafiti ili kuwezesha mipango bora ifanyike.

Mhe. Spika, vipaumbele hivi vimewasilishwa kupitia Bajeti Kuu ya Serikali na Bajeti za Sekta husika na kujadiliwa kwa kina katika kikao hiki. Napenda kutoa wito kwa watendaji wote wa taasisi za umma kujituma, kuwa makini na kufanyakazi kwa uadilifu mkubwa ili kuhakikisha vipaumbele hivi vinatekelezwa ili tupige hatua zaidi za maendeleo.

Mhe. Spika, Serikali kwa upande wake itajitahidi kuona kwamba nyenzo, hasa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa vipaumbele hivi zinapatikana na kwa wakati. Hivyo, Serikali itaimarisha ukusanyaji wa mapato kutoka katika vyanzo vyake mbali mbali. Ili kufikia azma hii, hatuna budi kushirikiana katika ukusanyaji na usimamizi wa kodi. Nachukua nafasi hii kuwasisitiza wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla kuwa na utamaduni wa kulipa kodi na ada katika huduma zote za kiuchumi na kijamii ili kuiongezea mapato Serikali kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Sambamba na hili, Serikali itachukua hatua madhubuti za kudhibiti uvujaji wa mapato katika taasisi na maeneo yote. Katika kulifanyia kazi suala hili, ni vyema kwa viongozi na watendaji wa Serikali kufuata maadili ya kazi na kujiepusha na vitendo vya rushwa.

Mhe. Spika, sina haja ya kuelezea kwa urefu kuhusu malengo na mipango mbali mbali ya Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara na Taasisi zake kutokana na maelezo yanayohusiana na malengo pamoja na mipango kutolewa vya kutosha na Waheshimiwa Mawaziri, wakati wakiwasilisha hotuba za wizara zao za makadirio na matumizi kwa mwaka 2014/2015. Napenda tu kuwasisitiza Waheshimiwa Mawaziri, kuyasimamia malengo na mipango hiyo kuhakikisha kuwa inatekelezwa. Ningependa pia kuwasihi mawaziri na watendaji wao kusimamia vyema matumizi ya fedha walizoidhinishiwa na Baraza hili tukufu.

MAMBO YALIYOJITOKEZA BARAZANI:

Mhe. Spika, katika mkutano huu wa 16 wa Baraza la Nane la Wawakilishi, jumla ya maswali ya msingi 66 na maswali 183 ya nyongeza yaliulizwa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na kujibiwa na Waheshimiwa Mawaziri wa sekta husika. Maswali yote ya msingi na nyongeza yalikuwa na lengo la kuboresha utendaji wa Serikali katika kuwahudumia wananchi wake.Naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe, walioulizа na Waheshimiwa Mawaziri kwa majibu ya kutosheleza waliyoyatoa.

Mhe. Spika, kuanzia tarehe 14 Mei, 2014 hadi leo, tumesema sana. Waheshimiwa Mawaziri wamesema na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu nao wamesema. Mawaziri wamesema wakati waliposoma hotuba zao za bajeti, Wenyeviti wa Kamati mbali mbali nao wamesema wakati wa kusoma maoni ya Kamati zao kuhusiana na hotuba za bajeti za Wizara husika. Lakini Wajumbe wa Baraza lako tukufu nao pia wamesema kwa kutoa michango yao mbali mbali kuhusiana na hotuba hizo za bajeti zilizowasilishwa. Hivyo, wote tumesema sana. Lakini ni Mawaziri ambao wamesema zaidi wakati wa majumuisho na wakati wa kupitisha vifungu walipotakiwa kutoa ufafanuzi na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili tukufu. Kwa kweli kila mmoja wetu ndani ya Baraza hili alisema sana.

Mhe. Spika, Hotuba juu ya Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo Zanzibar 2014/2015 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2014/2015 ziliwasilishwa. Aidha, jumla ya Wizara 16 za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ziliwasilisha hotuba zake za Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2014/2015 na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu walipata nafasi ya kuzichangia hotuba hizo.

Mhe. Spika, kwa upande wa Mwelekeo wa Hali ya Uchumi na Mpango wa Maendeleo Zanzibar 2014/2015 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2014/2015, Waheshimiwa Wajumbe wameishauri Serikali kuteua miradi michache inayotekelezeka. Aidha, Wajumbe waliishauri Serikali kuendelea kutafuta vianzio vyengine vya mapato ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa shughuli zake. Pia, Waheshimiwa Wajumbe, waliishauri Serikali kuongeza udhibiti wa mapato na usimamizi wa matumizi ya fedha za Serikali.

Mhe. Spika, kwa upande wa kuchangia Hotuba za Mawizara, pamoja na mambo mengine Wajumbe waliishauri Serikali kusimamia mambo muhimu ikiwemo kuzipatia wizara vifaa na vitendea kazi, kusimamia uwajibikaji na utunzaji wa mali za Serikali na kufanya mapitio ya sheria na kuandaa sheria mpya ili kuleta ufanisi. Vile vile, Serikali imeelekezwa kutoa fursa sawa za ajira kwa makundi yote, kuimarisha maslahi ya wafanyakazi na kuimarisha huduma za kijamii kwa ujumla ikiwemo afya, elimu, maji, nishati ya umeme na miundombinu. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kuwa ushauri, michango na mapendekezo yao yamepokelewa na yatafanyiwa kazi ipasavyo.

Mhe. Spika, Miswada miwili (2) iliwasilishwa na kujadiliwa katika mkutano huu. Mswada wa kwanza ni Mswada wa Sheria ya Kutoza Kodi na Kubadilisha Baadhi ya Sheria za Fedha na Kodi Kuhusiana na Ukusanyaji na Udhibiti wa Mapato ya Serikali na Mambo Mengineyo Yanayohusiana na Hayo. Madhumuni ya Mswada huu ni kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato na udhibiti wa matumizi ya Serikali. Katika kuchangia Mswada huu Waheshimiwa

Wajumbe waliishauri Serikali kusimamia utekelezaji wa sheria hii na kuweka utaratibu mzuri wa kuyarejesha mapato ya ukusanyaji kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Mhe. Spika, mswada wa pili ni Mswada wa Sheria wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio ya Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2014/2025. Mswada huu ulikuwa na lengo la kuthibitisha matumizi ya fedha za Serikali yatakayofanywa kwa mwaka 2014/2015. Wengi wa Wajumbe waliochangia mswada huu walihimiza matumizi mazuri ya fedha za Serikali na Serikali imesikia elekezo hilo na itasimamia kwa nguvu zake zote.

Mhe. Spika, aidha, Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Kuanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi na Mambo Yanayohusiana na Hayo na Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Uuguzi na Wakunga Nam. 9 ya 1986 na kuanzisha badala yake Sheria mpya ya Uuguzi na Wakunga na Mambo Mengineyo Yanayohusianayo Hayo ilisomwa kwa mara ya kwanza katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, Baraza lako tukufu pia lilipokea taarifa ya utekelezaji wa haki za mtoto kwa mwaka 2013/2014. Ripoti hiyo ilikuwa na lengo la kupima utekelezaji wa kisekta kwa haki za mtoto kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Watoto Nam. 6 ya 2011 pamoja na mikataba ya Kikanda na Kimataifa inayohusu uhai, hifadhi, ustawi na maendeleo ya mtoto.

Taarifa hii inakwenda sambamba na maadhimisho ya siku ya mtoto wa Afrika ambapo kwa mwaka huu ilikuwa na kauli mbiu isemayo elimu bora isiyo na vikwazo ni haki ya kila mtoto. Tunatoa wito kwa jamii kuitekeleza kauli mbiu hii kwa vitengo kwa manufaa ya nchi yetu.

Mhe. Spika, siku sijazo na inawezekana ikawa kesho, tutaingia ndani ya mwezi Mtukufu wa Ramadhani ambapo Waislamu kote duniani watatekeleza ibada ya funga. Inasisitizwa katika mwezi huu kusameheana, kuhurumiana na kusaidiana ili kufikia lengo la mwezi huu kama ilivyoelezwa na Mwenyezi Mungu Mtukufu katika Qurani Aya 183 inayosema, *"Enyi mulioamini mfadharalishwa juu yenu kufunga kama walivyofadhalishwa waliopita kabla ya yenu ili mupate kuwa wacha Mungu"*.

Mhe. Spika, wote tunafahamu kuwa mwezi wa Ramadhani ni mwezi wa rehma, maughfira na toba. Waislamu wote tuutumie mwezi huu vizuri ili kuweza kupata fadhila zilizopo ndani yake kwa kuzingatia maadili ya mwezi huu ikiwemo kujisitiri vizuri na kujiepusha na tabia ya kula hadharini.

Mhe. Spika, katika mwezi huu ni vizuri kwa wafanyabiashara kuzingatia uuzaji wa bidhaa zao, kwani kuna tabia kwa baadhi ya wafanyabiashara kuufanya mwezi huu kuwa ni wa kupata faida kubwa kwa kupandisha bei za bidhaa na vyakula na hasa vinavyotumika katika mwezi huu. Hivyo, Serikali inatoa wito kwa wafanyabiashara wote kupunguza bei za bidhaa na vyakula na kuwa waangalifu na waadilifu katika matumizi ya vipimo ili kila Muislamu aweze kupata mahitaji muhimu ya mwezi huu kwa bei nafuu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, tunamuomba Mwenyezi Mungu atukubalie fungu na ibada zetu zote kwa mwezi Mtukufu na miezi mengine na atuwezesha kumaliza kwa salama na kusherehekea vizuri Sikukuu ya Edd El Fitri. Hivyo, tunawaomba wananchi kufanya ibada zao kwa amani na utulivu pamoja na kujiepusha na mambo yote yatakayopelekea kubatilisha funga zao pamoja na kuvunja sheria za nchi.

Mhe. Spika, ni vyema kwa wananchi wote kuufuta maagizo ya dini zetu hasa katika suala la kuhubiri umoja, amani na mshikamano. Hivyo, basi tuutumie mwezi huu wa Ramadhani kama darasa kwa kuhurumiana, kupendana na kusaidiana na tuziache tofauti zetu za kidini, rangi na ukabila zinazotawala na kutuharibia nchi yetu.

Mhe. Spika, kabla ya kuhitimisha hotuba yangu hii, napenda kuelezea masikitiko yangu kutokana na mahudhurio yetu hapa Barazani. Miongoni mwa kazi za msingi za Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi ni kuhudhuria vikao vyote vya Baraza bila ya kukosa. Isipokuwa kwa sababu za msingi zinazokubalika kwa mujibu wa Kanuni zetu. Kitendo cha kulazimika kwa Mhe. Spika, jana asubuhi kuahirisha Baraza kutokana na sababu ya mahudhurio yasiyodhirisha ni jambo lisilokubalika kidemokrasia, kiuchumi na kisiasa na baya zaidi tabia hii ya utoro inalidhalilisha Baraza letu tukufu mbele ya macho ya wananchi wetu waliotuchagua.

Sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ni macho, masikio na midomo ya wananchi tunaowawakilisha majimboni mwetu. Kitendo cha kutokuhudhuria vikao vya Baraza, maana yake tunawanyima wananchi wetu kusikia na kuona

mambo yao yakizungumzwa na kutafutiwa ufumbuzi unaofaa. Kiuchumi utoro huu unapelekea kuahirishwa kwa vikao vyetu vya Baraza, unapoteza fedha nyingi za wananchi wetu. Hatuoni kama ni jambo la dhihaka tunapopiga kelele kuwa Serikali inapoteza fedha za wananchi, wakati sisi wenyewe pia tunachangia upotevu huo. (*Makofi*)

Wengi wetu hapa ni wazazi na walezi. Mtoto anapotoroka darasani, mzazi pamoja na mwalimu wake anaweza kumpa adhabu ya mikwaju. Adhabu hizi tunazitoa kwa sababu tunaelewa upo uhusiano wa karibu kati ya utoro na matokeo ya masomo darasani. Mtoto mtoro huvuna matokeo mabaya darasani. (*Makofi*)

Hakuna tofauti ya athari yetu Barazani na ule wa darasani. Utoro wetu Barazani unasababisha matokeo mabaya ya utendaji wa kazi zetu ndani ya Baraza. Kazi ya kufanywa siku moja inaweza ikalala hadi siku ya pili. Huu sio ufanisi, huu ni ule usemi wa Mhe. Rais kuwa *"Business as usual"*.

Kama watoto wetu tunawapiga mikwaju kwa utoro, kuna haja na sisi kujiwekea adhabu kwa makosa yetu haya ya kutohudhuria vikao. Bila shaka Mhe. Spika, atabuni adhabu hiyo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa kumalizia hotuba yangu ninapenda kuchukua fursa hii, kwa mara nyengine tena kuwakumbusha wananchi juu ya suala la kudumisha amani, utulivu na mshikamano katika nchi yetu ili tuweze kujiletea maendeleo zaidi ya kiuchumi, kijamii, kisiasa, kiutamaduni kwa kutekeleza shughuli zetu za uzalishaji mali bila ya bughudha.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena ninapenda kuchuku fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa hekma na busara zako unazozitumia katika kuliongoza Baraza hili. Aidha, ninapenda kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa uvumilivu waliounesha kwa muda wote wa mkutano. Ninakushukuruni sana na ninawatakia safari njema ya kurejea majimboni kwenu kwa ajili ya kuwatumikia wananchi.

Pia, ninapongeza watendaji wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa jitihada zao katika kutimiza wajibu wao na kuleta maendeleo ya nchi.

Mhe. Spika, ninachukua nafasi hii kuvishukuru kwa dhati vyombo vya habari vyote hapa Zanzibar hasa Shirika la Habari la Zanzibar la *ZBC*, kupitia redio na televisheni ambavyo vilirusha moja kwa moja mtiririko mzima wa shughuli za Baraza na kuwawezesha wananchi wetu kufuatilia kwa makini matokeo yote yaliyojiri Barazani hapa. (*Makofi*)

Pia, ninawapongeza wakalimani wetu wa lugha za alama kwa kazi nzuri waliyofanya ya kutafsiri mawasiliano na mijadala katika kipindi chote cha Baraza lako na kuwawezesha wananchi wenzetu wenye matatizo ya kusikia kufuatilia shughuli za Baraza. (*Makofi*)

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naomba kutoa hoja ya kuliahirisha Baraza lako tukufu hadi siku ya Jumatano tarehe 22 Oktoba, 2014 saa tatu asubuhi panapomajaaliwa.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kwa hotuba hiyo ya kufungia mkutano wetu huu wa 16 ambao ulikuwa ni mkutano wa bajeti.

Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijatoa matangazo basi, hoja imetolewa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais na niiamue basi. Wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, kuahirisha mkutano wetu huu hadi tarehe 22 Oktoba, 2014 saa tatu barabara za asubuhi, wanyanyue mikono, wanaokataa.

Waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, nikushukuru kwa hotuba nzuri ambayo inahitimisha shughuli zetu za mkutano huu wa bajeti. Ninashukuru kwamba shughuli zote zimekwenda vizuri kwa sababu ya mashirikiano makubwa ambayo tumepeana katika shughuli zetu hizi. Ninawashukuru sana Waheshimiwa wote kwa ujumla kwa kazi nzuri, lakini pia, nishukuru Kamati mbali mbali ambao zilizoshughulikia bajeti hii mpaka kufikia kumaliza kwake.

Waheshimiwa Mawaziri ninawashukuru sana tumekuwa tupo tayari kujibu maswali na hoja mbali mbali za Waheshimiwa Wajumbe na hiyo ndio iliyofanikisha shughuli zetu kufikia muafaka huu. Shughuli hizi zimefanyika vizuri baada ya mashirikiano makubwa yenu Waheshimiwa Wajumbe pamoja na sisi tunaoongoza chombo hichi. Kwa hivyo, nichukue fursa hii kuwashukuru sana kuwashukuru Mhe. Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza na Makatibu wakiongozwa na Ndugu Yahya Khamis Hamad ambao mara zote wamekuwa tayari kuweka ratiba na shughuli za vikao vyetu kwenda vizuri. (*Makofi*)

Nisisahau kumshukuru sana Mhe. Waziri wa Fedha, kuwezesha mkutano wote huu kwenda vizuri bila ya kutuacha mkono, jambo ambalo ninategemea ataendelea kwa muda wote tukiwa tunaendelea na shughuli zetu za vikao na mikutano ya Baraza hili. (*Makofi*)

Niwashukuru sana ndugu zetu hawa waandishi wa habari wametusaidia sana kupeleka taarifa hizi kwa wananchi, hasa hasa ndugu zetu wa televisheni, lakini na waandishi wa habari wengine wote ambao wanahudhuria hapa. Mara hii ninawashukuru watendaji wengi wa Serikali wamekuwa wanahudhuria shughuli zetu ili kushuhudia maelekezo na mashauri ambayo yaliyokuwa yametolewa na Waheshimiwa Wajumbe.

Waheshimiwa Wajumbe, basi nichukue nafasi kwa niaba yenu na kwa niaba ya wananchi kuwashukuru sana kwa kazi nzuri. Maelekezo ya Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, hapana shaka tutarekebisha pale ambapo tumekosea kosea ili tuwe na ufanisi na mzuri zaidi.

Waheshimiwa, baada ya hayo basi nichukue nafasi hii kuwatakia mfungo mwema na familia zetu na ndio iliyokuwa nia ya kuharakisha shughuli kidogo kumaliza leo ili turudi kwenda kufunga na kufutari pamoja na familia zetu.

Baada ya hayo sasa nichukue nafasi hii kuahirisha Baraza hili hadi tarehe 22 Oktoba, 2014 saa 3.00 asubuhi Mungu akitujaalia.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

(Saa 6.35 Mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 22 Oktoba, 2014 saa 3.00 Asubuhi)

WIMBO WA TAIFA